Jumanne Julai 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580640

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11


**Fatma** Karume akwaa kizingiti kingine kortini cha kurejeshewa leseni

UKURASA 4



**TCU** yafungua dirisha maombi 90,000 mwaka wa 2021/22

UKURASA 2



# Warioba awasha moto Katiba mpya

UK. 2

**Awataka** viongozi kuwa wasikilizaji zaidi kero za wananchi...

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### DCI ATOA MAELEKEZO UDHIBITI MOTO SHULENI

KUTOKANA na kuibuka kwa matukio ya moto kwenye shule, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camillus Wambura, ameziagiza kamati za shule kuweka ulinzi katika maeneo ya shule, mabweni na jirani...

UKURASA WA 16

### MWALIMU ASIMAMISHWA KAZI TUHUMA ZA KUMTUSI RAIS

NAIBU Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amemsimamisha kazi mwalimu wa Shule ya Sekondari Momba, Shera Mwangoka, kwa tuhuma za kumtukana Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ...



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza kwa njia ya mtandao na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya (EU), Charles Michel, Ikulu jijini Dodoma, jana kuhusu uhusiano kati ya Tanzania na **EU. PICHA: IKULU**

## Simbachawene atoa agizo sokoni Kariakoo

UKURASA 4

## EU yaimwagia Tanzania mabilioni

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA YAWEKA REKODI MIAKA 42** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# TCU yafungua dirisha maombi kwa 2021/22

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefungua dirisha la maombi ya udahili wa Shahada ya Kwanza, katika taasisi za elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2021/22 huku kukiwa na ongezeko la watakaodahiliwa.

Idadi ya wataodahiliwa mwaka huu wa fedha 2021/22 imeongezeka na kufikia 90,000 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/21 ambapo walikuwa ni 87,934.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alitangaza jana jijini Dar es Salaam kufunguliwa kwa dirisha hilo kuanzia siku hiyo na linatarajia kufungwa Agosti 5, mwaka huu.

"Tume imefungua dirisha la maombi ya udahili kwa waombaji wa Shahada ya Kwanza kuanzia Julai 12, mwaka huu badala ya Julai 15, mwaka huu iliyopangwa awali, dirisha hili litakuwa wazi hadi Agosti 5, mwaka huu," alisema.

Alisema tume inawahimiza waombaji wote wa udahili kuendelea kupata taarifa sahihi kupitia tovuti ya TCU iliyoruhusiwa kudahili wanafunzi.

Pia alisema TCU inawahimiza waombaji wa udahili na wananchi kwa ujumla kutembelea Maonyesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yanayotarajia kufunguliwa rasmi Julai 26, mwaka huu ili waweze kuonana na vyuo mbalimbali vya elimu ya juu.

Prof. Kihampa alifafanua kuwa maombi ya udahili yanahusu makundi matatu ambayo ni wenye sifa stahiki stashahada au sifa linganifu, sifa stahili za kidato cha sita, wenye sifa stahili za cheti cha awali ya Chuo Kikuu cha Tanzania.

"Mambo ya kuzingatia waombaji ni pamoja na kusoma mwongozo wa udahili uliotolewa na tume, kutuma maombi moja kwa moja chuoni kupitia mifumo ya kielektroniki, kuwasiliana na vyuo moja kwa moja ili kupata taarifa," alisisitiza.

Pia alisema kwa waombaji wenye vyeti vilivyotolewa na mabaraza ya mitihani nje ya nchi waviwasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani (NECTA) kwa vyeti vya elimu ya sekondari au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi NACTE) kwa vyeti vya stashahada ili kupata ithibaki ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kutuma maombi ya udahili," alisema.

Prof. Kihampa aliwasisitizia wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai kutoa huduma ya namna ya kujiunga na vyuo.



Watumishi wapya 82 wa Idara ya Afya na Elimu waliopangiwa kazi Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara wakijaza mikataba yao ya kazi baada ya kuripoti wilayani humo, kwa ajili ya kuanza kazi kwenye vituo vyao. Watumishi hao 62 ni walimu na 20 wa Idara ya Afya walikusanyika katika ofisi ya za halmashauri jana. **PICHA: HAMIS NASRI**

# Warioba awasha moto Katiba mpya

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba, amepigilia msumari kuhusu umuhimu wa Katiba mpya, na kutaka maoni ya wananchi yasipuuzwe kwa kuwa ndiyo mara yao kwanza walishirikishwa kuitengeneza.

Akihojiwa jana kwenye kipindi cha dakika 45 kinachorushwa hewani na Kituo cha Televisheni cha ITV, Jaji Warioba alisema ni muhimu mchakato wa Katiba mpya ukakamilishwa kwa kufikiria hatua ya kuchukua kuanzia ilipoishia mwaka 2014.

Alisema Katiba ni muhimu na imefika hatua kubwa ya kuwa na katiba mpya, kwani sheria na Tume iliundwa ili kupata maoni ya wananchi na ilizunguka nchi nzima kuyakusanya, na mambo yaliyokuwapo katika Rasimu ya Tume yalichukuliwa Bunge Maalum la Katiba yalitokana na maoni ya wananchi.

Jaji Warioba ambaye ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, alisema katiba za zamani walikuwa hawaulizwi wananchi, na kwamba kwa mara ya kwanza ya mwaka 2014 iliyoandaliwa ilipata maoni ya wananchi, hivyo maoni ya wananchi yasidharauliwe.

"Usije ukasema Katiba siyo muhimu wakati wananchi wanasema ni muhimu, tulipofikia ni hatua muhimu tunachotakiwa ni kutafakari kwamba tunamaliza vipi na lini, hata nilipomsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan, hakusema kwamba tusimalizie hiyo, anazungumzia lini."

"Na mimi naona kwa sasa hivi ni lazima tufikirie hivi ni lini tunatakiwa tukamilishe, tutumie utaratibu gani. Mwaka 2014 ilikuwa twende kupata maoni ya wananchi, lakini kwa mazingira ya wakati ule haikuwezekana sasa muda umepita inabidi ile Katiba inayopendekezwa ifanyiwe marekebisho," alisema.

"Wanaosema wanataka Katiba ya wananchi wakati mwingine nasikiliza sana hawa wanataka katiba ya wananchi au wanataka katiba ya wanasiasa kwa sababu wanachozungumzia sana ni Tume Huru ya Uchaguzi, Rais kuchaguliwa kwa asilimia zaidi ya 50, matokeo ya Rais kuwe na uwezekano wa kupeleka malalamiko mahakamani na kuwa na mgombea huru," alibainisha.

Kwa mujibu wa Jaji Warioba, mambo hayo ni muhimu, lakini msisitizo wa wananchi ilikuwa ni hiyo, wananchi walikuwa na mambo mengine waliyosisitiza mojawapo kuporomoka kwa maadili, ndiyo maana kumekuwa na rushwa, ufisadi na hakuna maadili, hivyo walisema ni lazima jambo hilo liingizwe kwenye Katiba.

Aidha, alisema walizungumzia tunu za taifa za misingi na miiko ya uongozi, haki za binadamu na malengo ya taifa, hivyo kwa kuwa Rais alikubali kukutana na wanasiasa wa vyama vya upinzani wazungumzie Katiba ya aina gani wanayoitoa kwa wananchi na kwa kipindi gani waipeleke.

"Ukiangalia mazingira yenyewe hatuwezi kuipata Katiba mwaka huu, kwa sababu inabidi twende kwa wananchi na hiki siyo kipindi cha kukusanya kwa sababu kuna hatari ya Corona, ni lazima tuwe na msimamo wa kitaifa tuamue lini tutakamilisha hii ama tunakamilisha kila kitu kwa wakati mmoja ama tunachukua sehemu fulani fulani tunazikamilisha ikifika wakati fulani tunakamilisha yote," alisema.

"Mimi nadhani wengi wanajua umuhimu wa Katiba, ushauri wangu wanasiasa wakubali mwaliko wa Rais wawe tayari kuzungumza kwa makini siyo kwa mapambano kwa sababu hili ni suala linalohusu wananchi... wazungumze wakubaliane wakifanya hivyo itakuwa rahisi kupata ridhaa kwa wananchi," alisisitiza.

### VIONGOZI WASIKILIZE

"Mimi napenda utaratibu wake wa kukutana na wadau mbalimbali, na hayo yaliyopita yanaweza kuboreshwa jambo la kwanza ni mikutano iwe ya Rais anapokutana na wadau basi tulenge kwa wale anaokutana nao, isiwe ni nafasi ya watu wengine kueleza mambo yao.

"Tumeona katika mikutano hasa ule wa vijana walijitokeza viongozi wengi kuzungumza na ikachukua muda wa saa tatu hadi nne kabla Rais hajazungumza, wananchi wanataka wamsikilize Rais, ukichukua muda mrefu mtu hawezi kukaa, hivyo unapotokea mkutano wa Rais basi ufanywe kuwa wa Rais, hao wengine wana nafasi nyingine," alishauri.

Jaji Warioba alisema ni vyema anapokutana na wananchi ni vizuri akawasikiliza kwanza, na kwamba ilivyoonekana viongozi walizungumza zaidi. Aliongeza kuwa njia sahihi ni kama alivyokutana na sekta binafsi.

"Sikuhizi inaonekana kama mikutano ni ya viongozi, mimi ningependa kama si yeye basi wasaidizi wake waende wafanye hivyo kwa wananchi wa kawaida, tumezoea kusema wananchi waeleze kero zao, lakini ni vizuri tukasikiliza mawazo ya wananchi, na wakutane nao badala ya kuwahutubia wawasikilize, maana hawo ndio wanaishi na matatizo," alisema.

"Ukienda kijijini kote utakuta wana matatizo mengi kama ya kilimo, ufugaji, uvuvi, barabara, shule, zahanati na maji. Ni mengi na hayawezi kuisha kwa wakati mmoja, wakiwasikiliza wananchi watajua kipaumbele chao ni nini, ili wajue tuanzie wapi ili wapate nguvu za kujiendeleza," alisema.

# DCI atoa maagizo matukio ya moto shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUTOKANA na kuibuka kwa matukio ya moto kwenye shule, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camillus Wambura, ameziagiza kamati za shule kuweka ulinzi katika maeneo ya shule, mabweni na nyumba za jirani.

Wambura alitoa agizo hilo jana alipokuwa akitoa taarifa ya hali ya usalama nchini kwa vyombo vya habari, katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu.

Alisema kumekuwapo na matukio mbalimbali ya kuungua moto shule katika mikoa mbalimbali na kusababisha majeruhi na upotevu wa mali za wanafunzi.

"Naagiza viongozi wa shule kufanya ukaguzi wa miundombinu ya shule mara kwa mara pamoja na kuweka vizima moto," alisema.


Alisema wanapaswa kukagua kila mara maeneo yaliyo karibu na shule pamoja na jamii inayowazunguka pamoja na kuweka ulinzi katika majengo yao.

"Nawaomba kamati za shule kuweni makini na haya mambo mnahitajika kuweka ulinzi wa kutosha, huku Jeshi la Polisi likiendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha moto inayotokea katika shule," alisema.

Hata hivyo alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (TANESCO) wanaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini nini chanzo cha shule hizo kuungua moto kila mara.

"Morogoro ilitokea kuungua kwa shule mbili, moja ikiwa inamilikiwa na wakristo na nyingine inayomilikiwa na waislamu... inashangaza sana matukio hayo, nawaomba kamati za shule zitekeleze hili nililowaagiza," alisema.

Mwishoni mwa wiki, Shule ya Sekondari ya Charlotte na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya At-Taaun inayomilikiwa na taasisi ya kiislamu ziliungua moto kwenye mabweni ya wanafunzi.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo (kushoto), akiwa na Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), Justina Mashiba, wakionyesha baadhi ya huduma za Shirika la Posta wanazozitoa walipotembelea banda lao katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA MIRAJI MSALA**

# Benki EU yaipa Tanzania bil. 137/-

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameshukuru Umoja wa Ulaya (EU) kwa ushirikiano katika masuala ya maendeleo ya jamii na kuwekeza katika miradi ya miundombinu kupitia Benki ya Uwekezaji ya EU.

Alisema Benki hiyo imetoa Euro milioni 50 (Sh. bilioni 132.022) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa baadhi ya viwanja vya ndege vya mikoani.

Pia, katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita Tanzania na Umoja wa Ulaya zimesaini makubaliano ya msaada wa Euro milioni 111.5 kwa ajili ya kuboresha miradi ya sekta ya nishati hususani matumizi ya majiko banifu, uongezaji thamani mazao ya nyuki, kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha usalama wa chakula.

Rais Samia alisema hayo jana wakati akizungumza kwa njia ya mtandao na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, Ikulu jijini Dodoma, kuhusu uhusiano kati ya Tanzania na Umoja huo.

Michel amempongeza Rais Samia kwa hatua mbalimbali anazochukua tangu kushika hatamu ya uongozi na kumhakikishia kuwa Umoja wa Ulaya (EU), utaendelea kuwa mshirika muhimu na wa kimkakati wa maendeleo nchini Tanzania na kikanda.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, ilisema pia Michel amempongeza Rais Samia kwa jitihada anazochukua kupambana na ugonjwa wa corona.

Vilevile, amemweleza kuwa EU tayari inashirikiana na viwanda mbalimbali vinavyozalisha chanjo barani Afrika kwa kuvijengea uwezo na kuongeza kuwa iwapo Tanzania itahitaji msaada huo EU iko tayari kuisaidia.

Kwa upande wake Rais Samia kadhalika, alisema kwa sasa serikali inaendelea na uboreshaji wa mazingira bora ya uwekezaji kwa sekta binafsi ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) wa Tanzania.

Alimhakikishia Michel kuwa utawala wake utasimamia na kuimarisha demokrasia, utawala bora na haki za msingi za binadamu.

Kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona, Rais Samia amemtaarifu Rais huyo wa Baraza la EU, Michel, kuwa Tanzania tayari imeshajiunga na Mpango wa Kimataifa wa ugawaji wa chanjo kwa nchi maskini (COVAX facility) na ina mpango wake wa taifa wa kupambana na corona unaoainisha mahitaji ya nchi na kwamba itawasilisha mahitaji yake kwa EU ili kupata msaada.

Rais Samia pia, ameshukuru kupokea mwaliko wa kutembelea Umoja wa Ulaya na kumtumia salamu Rais wa Umoja huo, Ursula von der Leyen.

# Agizo la barakoa, 'level seat' lakwama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

AGIZO la uvaaji barakoa kwa wafanyabiashara wote kwenye masoko na kupakia abiria kulingana na idadi ya viti (level seat), hususan daladala lililotolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, limeshindwa kutekelezwa.

Nipashe ilitembelea jana kwenye masoko ya jijini Dodoma na kituo cha daladala Sabasaba, na kubaini wafanyabiashara kufanya shughuli zao bila kuvaa barakoa, huku daladala zikijaza abiria wengi kuliko idadi ya viti na kutokuwapo kwa vifaa kwa ajili ya kunawa mikono.

Hata hivyo, madereva na makodakta wa daladala waliozungumza na Nipashe, walisema wanalazimika kujaza abiria kutokana na kiasi cha fedha kinachotakiwa kuwasilishwa kwa wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri. Juma Hassan, dereva wa daladala inayofanya safari za Sabasaba kwenda Nzunguni jijini hapa, alisema serikali inatakiwa kutoa elimu pia kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri ambao wamekuwa wanahitaji kiwango cha fedha walizopanga kikamilike bila kujali nini kimetokea.

"Sisi hatupingi agizo la Mkuu wa Mkoa ambalo ameagiza kwenye daladala zote kuwe na 'level seat', tatizo lililopo kwa wamiliki wanataka kiwango cha fedha tulizokubaliana nazo zitimie na siyo vinginevyo," alisema.

Mzee Kajeli, kondakta wa daladala zinazofanya safari Nkuhungu hadi stendi ya Sabasaba, alisema agizo la Mkuu wa Mkoa lisiishie kwao, pia litolewe kwenye minada na mikusanyiko mbalimbali.

Juzi, Mtaka alitangaza kuanzia jana wafanyabiashara wote wa masoko, minada na maeneo yenye mikusanyiko kuvaa barakoa na atakayekaidi, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Pia, alisema uongozi wa Mkoa huo umepiga marufuku wamiliki wa vyombo vya usafiri hususani daladala kupakia abiria zaidi ya idadi ya viti.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATA YA MBAGALA KUU, HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM NA KATA YA MCHEMO, HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA, MKOA WA MTWARA, TANZANIA BARA TAREHE 18/07/2021.**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Kata ya Mbagala Kuu, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Jijini Dar es salaam na Kata ya Mchemo, Halmashauri ya Wilaya ya Newala, Mkoani Mtwara Tanzania Bara kuwa kutakuwa na Uchaguzi Mdogo wa Udiwani siku ya Jumapili, tarehe 18/07/2021. Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) Asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) jioni.

1. **SIKU** : Wananchi watapiga Kura siku ya Jumapili tarehe 18/07/2021
2. **VITUO** : Zoezi la Upigaji Kura litafanyika katika vituo vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.
3. **MUDA** : Vituo vitafunguliwa saa kamili (1:00) Asubuhi na kufungwa saa kumi ( 10:00) Jioni

**Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi.**

1. Watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura mwaka 2020 na wana kadi za Kupigia Kura.
2. Aidha, waliopoteza kadi zao za kupigia kura au kuharibika, wanaruhusiwa kutumia hati ya kusafiria, Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Taifa ambacho majina yote matatu yanafanana na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
3. Mpiga Kura anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni.
4. Watu wenye Ulemavu, Wazee, Akinamama Wajawazito na wanaonyonyesha walioenda na watoto wao vituoni watapewa kipaumbele.
5. Mpiga Kura anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Kituo.
6. Baada ya kumaliza kupiga kura, Mpiga Kura anatakiwa kurudi nyumbani.

**Wilson Mahera Charles**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

216354802

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Eneo la uwekezaji Njedengwa, Kitalu D, Kiwanja Na. 4, Uchaguzi House, S. L. P 358, Dodoma. Barua Pepe:uchaguzi@nec.go.tz, info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.**

## Simbachawene aagiza kila soko kuwa na maji

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewaagiza wakuu wa mikoa nchini, kuhakikisha kila soko lina miundombinu wezeshi ikiwamo maji, ili kurahisisha uokoaji yanapotokea majanga.

Amesema shughuli kwenye Soko Kuu la Kariakoo ambalo liliungua moto juzi, zitaendelea kusitishwa hadi tathmini ya uchunguzi itakopotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Dar es Salaam, kujiridhisha.

Simbachawene aliyasema hayo jana alipotembelea soko hilo, kuona hali halisi na kwamba tukio hilo limetoa funzo kwa serikali kufanya ukaguzi kwenye majengo ya umma ikiwamo masoko, yawe na maji, njia zinazopitika kufanya uokoaji.

"Hili bado ni eneo hatarishi lililo chini ya Jeshi la Zimamoto na kamati ya ulinzi. Tathmini haijafanyika shughuli hazitaendelea hadi wajiridhishe... Sasa soko lijipange katika utaratibu mzuri.

Wenzetu Wizara ya Maji, wahakikishe maji yanapatikana pamoja na 'fire hydrant' kuwepo alarm pia, hata kama miundombinu ni ya zamani iboreshwe. Ndani ya siku chache shule, soko limeungua tujipange," alisema Simbachawene.

Waziri huyo ambaye aliongozana na uongozi wa mkoa, wilaya na taasisi mbalimbali akiwamo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema tayari ameomba ushirikiano wa ukaguzi madhara kiafya akiwamo Mkemia Mkuu wa Serikali, kubaini athari za moshi unaoendelea kutoka ndani ya jengo.

"Moto umebaki maeneo mawili na bado biashara hazitaanza. Biashara zitaanza kama Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa, ikijiridhisha," alisema Makalla.

Rais wa Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Paul Koyi, alisema wafanyabiashara wawe na uvumilivu huku serikali na taasisi hiyo ikisubiri tathmini namna ya kuwarejesha kwenye maeneo yao.

"Kariakoo niwahakikishie tupo pamoja, tutakaa chini na kuangalia namna ya kuwarudisha wenzetu, baada ya janga hili. Nitoe pole kwa wafanyabiashara wenzetu," alisema Koyi.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Soko Kuu Kariakoo, John Shao, alisema wamesikitishwa na tukio hilo ambalo limewapa hasara wakiomba serikali kuwafikiria waliokopa benki na namna ya kurejesha biashara zao.

Kamishna Msaidizi kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa Dar es Salaam, Bakari Mrisho alisema tatizo lilikuwapo katika shughuli ya uzimaji moto kutokana na uhaba wa maji sokoni.

"Changamoto ya maji na elimu duni kwa wananchi juu ya majanga ya moto, ndio sababu Afrika kwenye majanga kama haya watu ndio wanakimbilia badala ya kuyakimbia, barabara za kupitia hakuna, wamejaa watu, wafanyabiashara, hakuna uwazi wala upenyo magari ya Zimamoto kupitia," Kamanda Mrisho.

# Fatma Karume akwaa kizingiti kingine kortini

**Na Kulwa Mzee**

JAMHURI imewasilisha nia ya kukata rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu uliotengua uamuzi wa kumfuta katika orodha ya mawakili, Fatma Karume.

Nia hiyo ya kukata rufani imekwamisha maombi ya Fatma kupitia Wakili wake, Peter Kibatala, ya kutaka Msajili wa Mahakama Kuu atoe amri na kuelekeza mteja wake aendelee kufanya kazi ya uwakili.

Wakili Kibatala aliandika barua kwa Msajili wa Mahakama Kuu, akiomba mteja wao Karume aendelee kufanya kazi ya uwakili kama Mahakama hiyo ilivyoamuru Juni 21, mwaka huu. Katika barua hiyo aliomba Msajili wa Mahakama Kuu aamuru na kuelekeza kwamba leseni namba 848 ya Karume iliyozuiliwa iendelee kutumika kwa kazi ya uwakili.

Msajili Sharmilla Sarwatt katika majibu yake aliwafahamisha kwamba mlalamikiwa Jamhuri katika rufani namba 2/2020 iliyokuwa Mahakama Kuu aliwasilisha nia ya kukata rufani akipinga uamuzi wa Mahakama hiyo uliotolewa Juni 21, mwaka huu.

Mahakama Kuu Masjala Kuu ilitengua uamuzi wa Kamati ya Mawakili iliyomfuta Karume katika orodha ya mawakili nchini. Uamuzi huo ulitolewa na jopo la majaji watatu wa Mahakama Kuu, likiongozwa na Jaji Issa Maige, Jaji Deo John Nangela na Jaji Edwin Kakolaki.

Jopo hilo lilitoa uamuzi huo kutokana na rufani iliyokatwa na Karume akipinga uamuzi wa kusimamishwa uwakili uliotolewa na Kamati ya Mawakili.

Karume alifutiwa uwakili na kamati hiyo Septemba 23, mwaka 2020 kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na Adelardus Kilangi, akimtuhumu kukiuka maadili ya taaluma kwa kutumia lugha ya kumdhalilisha wakati akiwasili hoja za maandishi katika shauri alilokuwa akimwakilisha mteja wake Ado Shaibu.

Jaji Kiongozi, Dk. Eliezer Feleshi, alimsimamisha uwakili kwa muda Karume kutokana na malalamiko yaliyowasilishwa na mawakili wa serikali katika kesi waliyokuwa wakimwakilisha Profesa Kilangi na Dk. John Magufuli na kuelekeza malalamiko hayo yasikilizwe na kamati.

Mahakama Kuu katika uamuzi wake wa kutengua ilikubaliana na sababu moja pekee ya rufani hiyo ambayo ilitosha kutengua uamuzi wa kamati hiyo.

Katika sababu hiyo ambayo Mahakama Kuu ilikubaliana nayo, Karume kupitia kwa wakili wake alidai kuwa kamati haikuwa na mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya Profesa Kilangi kwa kuwa ilikuwa inakiuka uamuzi wa Jaji Kiongozi.

Mawakili wanaomtetea Fatma, Peter Kibatala na Dk. Rugemeleza Nshalla walipinga uamuzi wa kumsimamisha uwakili mteja wao uliotolewa na Kamati ya Maadili baada ya Jaji Kiongozi, Eliezer Feleshi mwaka 2019 kuelekeza shauri hilo likasikilizwe na kamati hiyo na kabla ya kufanya hivyo kamati ilianza kusikiliza malalamiko ya Kilangi.

Jopo hilo baada ya kupitia hoja mbalimbali zilizowasilishwa lilitengua adhabu ya kufutiwa uwakili na kutoa amri kwa ajili ya utekelezaji.

Mahakama katika uamuzi wake iliamuru malalamiko yapelekwe katika Kamati ya Mawakili watakaotoa uamuzi dhidi ya Karume.

"Kwa uamuzi huo Fatma atakuwa na nafasi ya kujitetea, amerudishiwa uwakili wake, hivyo anayo haki ya kujitetea," alisema Dk. Rugemeleza Nshalla. Pia Mahakama Kuu iliamuru Msajili wa Mahakama hiyo ndio apeleke malalamiko kwenye kamati ya mawakili.

Mahakama Kuu ilifuta mwenendo wote wa kamati ya maadili ya mawakili na kwamba hoja zao za kupinga kufutiwa uwakili Karume zilikuwa 13.

Karume alisimamishwa kazi huku sababu yake ikitajwa kuwa kile alichokizungumza katika kesi iliyofunguliwa na Ado.

Anadaiwa kuandika "hata iwapo kesi hii itashindwa, ataendelea kupambana nayo, rais akiondoka madarakani mwaka 2020 au kama ataondoka 2025 au kama mahakama itabadilika ataendelea kupambana".




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 220 kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia kutokomeza tatizo la miguu pinde kwa Watanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makatibu waahidi kurudisha heshima SMZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKATIBU wakuu na Manaibu Katibu walioapishwa jana baada ya kuteuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kushika nyadhifa hizo, wameahidi kufanya kazi kwa uadilifu na ufanisi ili kurudisha heshima kwa aliyewateua.

Waliyasema hayo jana Ikulu jijini Zanzibar wakati wakizungumza na waandishi wa habari.

Walisema watafanya kazi kwa bidii na kuisaidia nchi kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Walioapishwa ni Mussa Haji Ali kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Dk. Habiba Hassan Omar, kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Issa Mahfoudh Haji kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Wengine ni Aboud Hassan Mwinyi, kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango anayeshughulikia Fedha na Mipango na Mikidad Mbarouk Mzee kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema Rais amemwamini na kumkabidhi kazi hiyo ambayo inahitaji utekelezaji na uadilifu mkubwa na kuahidi kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa kazi, sheria, kanuni na utaratibu ili kuleta maendeleo ya Zanzibar.

Alisema wizara aliyopewa amejipanga kuvifanyia kazi kwa umakini ikiwamo kuondoa changamoto, migogoro katika sehemu za kazi hasa kwa waajiri na waajiriwa.

Kwa upande wa sekta ya uchumi, alisema atahakikisha wanashirikiana pamoja na watendaji wingine wa wizara yake katika eneo la uchumi ili kusogeza mbele uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Dk. Habiba alisema kwa upande wa uwekezaji amejipanga kuhakikisha uwekezaji unakwenda mbele kwa wawekezaji wenyewe na kile wanachokiwekeza nchini.

Naye Aboud Hassan Mwinyi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, anayeshughulikia Fedha na Mipango, alisema amepewa dhamana kubwa ya fedha na hatokuwa tayari kuona wizara yoyote inafanya ubadhirifu wa fedha za umma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jeshi la Polisi liongeze nguvu kupambana na uhalifu nchini

**HIVI** karibuni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema Jeshi la Polisi limefanikiwa kunyamazisha majambazi kimya kimya kwenye maeneo mengi.

Aidha, alithibitisha kuibuka kwa wimbi la ujambazi katika miji ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza, na kwamba operesheni ya kwanza kupambana na majambazi hao imefanikiwa kwa ufanisi mkubwa na sasa awamu ya pili imeanza huku akituma salamu kwa wanaodhani kufanya ujambazi ni njia sahihi ya kujipatia kipato waache mara moja.

Kauli ya Waziri imekuja wakati kwenye maeneo mengi ujambazi na wizi umekuwa kero kubwa na sasa waporaji wa kutumia pikipiki wamerejea, jambo linalohitaji nguvu ya ziada kwa jeshi hilo.

Uporaji unaofanyika kwa kutumia pikipiki ni kupora pochi, simu za watu kwenye vituo vya daladala, barabarani au kwenye vyombo vya usafiri.

Pia, wizi wa vioo na vifaa vingine huku magari yakitembea umerudi hasa yakiwa kwenye foleni, jambo linaloashiria kuwa bado inahitajika nguvu kubwa kukabiliana na wahalifu hawa ambao waziri amesema wanaijaribu serikali.

Mathalani, kwa sasa kwenye mitaa mingi watu wanaibiwa majumbani kwa maana ya kuvunja kuiba TV na vitu vingine vya ndani, pamoja na wizi wa magari ambao ulibaki historia.

Jana limetokea tukio eneo la Temeke baada ya wezi kuingia nyumbani kwa mtu na kujaribu kuiba gari, lakini wahusika waliwashtukia mapema, huku matukio ya watu kuibiwa vifaa vya magari yakiongezeka kwa kasi.

Mathalani, eneo la Kaseni, Kifula, Kisanjuni na Msangeni wilayani Mwanga, umeingia wizi mpya wa kuvunja madirisha kupuliza dawa na kuiba vitu vya ndani kama TV na vinginevyo umeshika kasi, na ndani ya wiki moja kuna matukio sita yameripotiwa kutokea kwenye nyumba tofauti.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, lilieleza kukamata watuhumiwa zaidi ya 100 wa wizi wa vifaa vya magari na vyombo vya usafiri na kuonyesha vifaa vilivyodaiwa kuibiwa maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Wizi unaripotiwa pia maeneo ya Tegeta, Salasala, Boko, Mikocheni, Tabata na kwingine, na kwa sasa ni kawaida mnapokuwa watu 10 kwenye kundi moja watatu au wanne utawasikia wakieleza kuwapo kwa matukio ya wizi kwenye nyumba zao.

Ndani ya miaka sita matukio ya uhalifu yalipungua nchini na kwisha kabisa hasa uporaji, lakini kwa sasa umerudi kwa kasi kubwa.

Ni muhimu sana mbinu zilizotumika kudhibiti hali hiyo kwa miaka sita ikatumika kuhakikisha matukio haya yanakuwa historia.

Kuna miaka vikundi vya ujambazi vilikuwa vingi ikiwamo kuwa na wafadhili na kulifanyika operesheni ya kukamata wafadhili wake na vinara hasa kwa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza, na kufanikiwa kudhibiti wizi wa magari.

Aidha, ni muhimu kurudi kwenye polisi jamii katika kudhibiti uhalifu kwenye mitaa, ikiwamo askari wa pikipiki maarufu kama Tigo, kufanya kazi hiyo, ikiwamo kumaliza mtandao wa uhalifu ambao wakati mwingine baadhi ya askari hulaumiwa kwa madai ya kuhusika kutoa taarifa za watoa siri.

Wajibu wa kulinda raia na mali zao ni wa Jeshi la Polisi, ni muhimu kutimiza kwa ufanisi mkubwa kuhakikisha kuwa jamii inakuwa salama muda wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu hii inatibu kutokujua kusoma wala kuandika



**Na Sabato Kasika**

**ELIMU** ya awali ni hatua ya mwanzo ya kumjengea mtoto uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu.

Ni mwanzo ili hata anapoanza ngazi ya pili awe na msingi wa kumwezesha kufanya vizuri zaidi katika masomo baada ya kujua mazingira.

Umuhimu wa elimu hiyo, unawalazimu wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka watoto wao katika hatua hiyo ya awali, kabla ya kuendelea na shule ya msingi.

Kutokana na umuhimu wa elimu ya awali, serikali imeelekeza kila shule ya msingi kuwa na darasa la elimu hiyo, ili watoto wote ambao hawajafikia umri wa kuanza darasa la kwanza, waanzie 'kupikwa' huko.

Hatua hiyo inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika, kwani watakuwa wamepata msingi bora tangu awali kuliko kujifunza wanapoamza darasa la kwanza.

Serikali imebeba jukumu la kutoa elimu bure tangu shule za awali hadi sekondari, hivyo kama wataendelea kuwapo wazazi na walezi wasioona umuhimu wa elimu, wanaweza kuharibu ndoto za watoto wao.

Ikumbukwe Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's) hususani katika lengo namba 4 la elimu, hivyo ni muhimu jamii kusaidiana na serikali kusimamia na kutimiza lengo hilo kwa kishindo.

Malengo hayo yanayofikiwa mwaka 2030, yanagusa mambo mengi ikiwamo ubora wa elimu, ikiwa ni kujenga na kuboresha miundombinu ambayo itachangia mazingira bora ya kujifunza kwa watoto kwa wote.

Inaelezwa kuwa katika nchi maskini duniani, watoto na vijana wenye umri wa kwenda shule, hukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo watoto wa kike kutokwenda shule kwa sababu nyingi ikiwamo ndoa za kulazimishwa.

Vilevile wanaoishi na ulemavu hukwama kwenda shule kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu toshelevu kwa mahitaji yao na hata wale wanaokwenda hukabiliwa na mazingira duni ya kusoma.

Ni vyema kila mzazi na walezi kuhakikisha watoto wanapata elimu ya awali kwa kuwaondolea vikwazo ambavyo husababisha wasipate msingi huo muhimu.

Ikumbukwe kuwapo darasa la elimu ya awali kunasaidia watoto kuanza elimu ya msingi wakiwa tayari wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu, kuliko kuwaacha walivyo na kujikuta wakiwa 'mbumbumbu' wanapoingia la kwanza.

Mtoto kuhitimu darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika, ni matokeo ya kutoanzishwa elimu ya awali ambayo ni msingi bora kwake unaompa uelewa mapema kabla kuanza elimu ya msingi.

Wazazi na walezi wakumbuke kuwa, uhaba wa madarasa katika shule za serikali, unasababisha wanafunzi kurundikana katika chumba kimoja na kuufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa mgumu.

Kwa mazingira kama hayo, si rahisi mwalimu kumfikia kila mwanafunzi ama wanafunzi wote kumuelewa, hivyo wale ambao watakuwa hawajapitia elimu ya awali wanaweza wasijue kusoma na kuandika hadi wanahitimu darasa la saba.

Katika elimu ya awali, mwalimu unapaswa kumwezesha mtoto kujenga umahiri kupitia shughuli zilizobainishwa, mbinu, zana stahiki za kufundishia na kujifunzia na kupima maendeleo ya mtoto hatua kwa hatua.

Hayo ni baadhi ya yaliyomo kwenye mwongozo Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambayo imeandaa Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali ambao unalenga kuwajengea watoto umahiri uliokusudiwa.

Mwongozo huo unatoa maelezo kuhusu uchambuzi wa mtaala na ujifunzaji na ufundishaji katika elimu ya awali.

Aidha, unahusu upimaji wa maendeleo ya elimu ya mtoto wa awali na pia huwapatia walimu maelezo kuhusu maandalizi ya ufundishaji na namna ya kuwezesha ujenzi wa umahiri ambao mtoto wa elimu ya awali anastahili kuujenga.

## Ufafanuzi ukataji tiketi stendi ya Magufuli

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imetoa ufafanuzi kwa wamiliki wa mabasi kutumia sehemu zisizo rasmi ndani ya stendi ya Magufuli, wakati wa kuwakatia abiria tiketi badala ya kutumia ofisi zilizotengwa kwa ajili ya suala hilo.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa kituo hicho kilichopo Mbezi Luis, mkoani Dar es Salaam, Maira Chilosa, alisema sababu ya wamiliki hao kutoa huduma ya kukata tiketi kwenye meza inatokana na kusubiri ofisi zikamilike.

Alisema sehemu ambazo wanazitumia kwa sasa ni kwa muda mfupi wakati jitihada za kukamilisha ukarabati wa vyumba vilivyotengwa kwa ajili hiyo ukiendelea.

"Vipo vyumba baadhi ambavyo tayari vimeisha kamilika, lakini hatuwezi kuwapa wengine na wengine wakaachwa hakuna atakayekubali aende kule juu halafu wengine wabaki pale chini, wakiondoka wanatakiwa waondoke wote ndiyo maana tunasubiri zikamilike zote ili tukianza kuzigawa tuzigawe kwa wote na zinatarajiwa kukamilika muda sio mrefu," alisema Chilosa.

Aliwataka wamiliki wa mabasi kuondoa wasiwasi kwa kuwa eneo hilo linajitosheleza, kila mmiliki aliyekamilisha vigezo vya kupatiwa ofisi atapata, zimewekwa kwa idadi itakayokidhi mahitaji ya watoa huduma.

Akizungumzia mabasi yanayofanya safari za mikoani, alisema kutokana na agizo lililotolewa na Mkuu wa mkoa huo, Amos Makalla, kuwa yote yashushe abiria ndani ya kituo hicho, wanapaswa kufuata utaratibu huo kwa kuwa stendi hiyo imewekwa miundombinu rafiki inayowezesha mabasi yote kuingia na kushusha watu kwa mpangilio mzuri.

Julai 9, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makalla alipofanya ziara katika kituo hicho na kusema katika mkoa huo serikali inatambua kituo cha mabasi kimoja ambacho ni cha Magufuli na kuagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha mabasi yote yanapakia na kushusha abiria ndani ya eneo hilo.

## Kichanga chakutwa kimekufa choo cha shule

**Na Said Hamdani,** LINDI

VITENDO vya ukatili dhidi ya watoto vinaendelea kushamiri katika Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, baada ya mtoto mwenye umri wa siku moja kutelekezwa na mama yake muda mfupi baada ya kujifungua.

Taarifa kutoka wilayani humo na kuthibitishwa na mamlaka husika ya serikali, zinaeleza kichanga hicho cha jinsi ya kike kimekutwa eneo la Shule ya Msingi Liwale na wapita njia asubuhi ya Julai 7, huku kikiwa kimeshafariki dunia.

Hili ni tukio la pili wilayani humo kutokea katika kipindi cha mwezi mmoja. Katika tukio lingine kichanga kingine chenye umri unaokadiriwa kuwa wa mwezi mmoja kilitupwa porini na mwili wake kubainika wiki moja baadaye baada ya mwanamke aliyefanya kitendo hicho kutiwa mbaroni na kumtaka aonyeshe eneo alikomtupia.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, baadhi ya mashuhuda wa mwili huyo, Ashura Yusufu, Juma Hemedi, Somoe Ally, Christina Kambona na Mohamedi Kindamba, walisema kichanga hicho kiliokotwa eneo la choo cha shule hiyo kikiwa kimeshafariki kutokana na kile walichoeleza kupigwa na baridi.

"Bado huyu dada hajafahamika jina wala eneo analoishi hapa Liwale," alisema mmoja wa mashuhuda hao.

Walisema baada ya kukikuta kichanga hicho walitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya kitongoji cha Liwale mjini, waliyemtaja kwa jina moja la Mpoto na baadaye Kituo cha Polisi cha Wilaya.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutelekezwa kwa kichanga hicho, na kueleza kwa upande wao wanaendelea kumsaka mtuhumiwa ili sheria ichukue mkondo wake.

# Daktari bingwa aonya wanaodai vidonge vya P2 kutibu Ukimwi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BAADHI ya wanaume mkoani Njombe wameshauriwa kuachana na imani potofu kuwa vidonge vya dharura vya kuzuia mimba P2 vinazuia maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa kufanya ngono zembe. Akizungumza na Nipashe jana, Daktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, Joseph Kimaro, alisema P2 ni dawa inayotumika kwa ajili ya kuzuia mimba kwa dharura tu.

"Dawa hii haina uhusiano wowote wa kuzuia kwa mwanamke yeyote au mwanaume asipate ugonjwa wa zinaa ...hii ni kwa ajili ya kuzuia mimba na inatumika kama njia ya dharura," alisema Kimaro.

Alisema endapo jambo hilo litaendelea, mtumiaji anajiweka kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama Ukimwi.

"Kama unavyofahamu Njombe Ukimwi upo kwa wingi, na akifanya ngono zembe huku akitegemea itamsaidia akimeza P2 asipate Ukimwi au asipate kaswende basi anakuwa anajidanganya mwenyewe," alisema.

Aliongeza: "Niseme kwamba wanaume wanaomeza P2 kuzuia Ukimwi au magonjwa ya zinaa ni kwamba wana imani potofu dhidi ya dawa hii, nishauri kwamba elimu ya afya itolewe kwa kundi hili la wanaume wanaotumia P2 kujikinga na maradhi mbalimbali ya zinaa, ukiwamo Ukimwi," alisema Dk. Kimaro.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

PURSUANT TO REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019 AND REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014.

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | |
| a) Monthly | FREE | FREE |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free<br>Above 5000 - 0.3% |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges<br>a) Monthly<br>b) Interm | **5000**<br>**5000+500 for each page** | **$5**<br>**$ 5+1 for each page** |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE<br>ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free<br>5000 to 10,000 - 0.3%<br>Above 10,000 - 0.5% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE<br>ABOVE 50 MIO--0.12% | **Upto 10,000- Free**<br>**> 10,000- 0.3%** |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 |
| 7. Cheque Return Charges | | |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | |
| 1. Cash Withdrawal | | |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA |
| **Mobile Banking Services** | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA |
| **H. LOCKERS RENT YEARLY** | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | |
| 3. BIG | 750,000.00 | |

| D. REMITTANCES | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Upto 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| above 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Upto 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| above 10,000 | NA | $30 |
| **E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000<br>5Mio to 10 Mio - 200,000<br>10 Mio to 25mio - 400,000<br>25 mn to 500 mio - 1.5%<br>>500mio--1.25%*<br>*minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100<br>5000 to 10,000 - $200<br>Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.5%<br>>500,000--1.25%*<br>*minimum 7,500 |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL--<br>>100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL--<br>>50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000<br>5 Mio to 10 Mio - 200,000<br>10Mio 25mio - 450,000<br>25 mn to 500 mio -1.8%<br>>500mio--1.5%*<br>*minimum 9mio | Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.8%<br>>500,000--1.5%*<br>*minimum 9000 |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000<br>>100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25<br>>50,000 ----50 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS 120,000 | USD 50 |
| 6.Pre-payment penalty | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |

**OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million up to 100 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 up to USD 100,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| NAME | TITTLE | SIGNATURE | DATE |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 10-07-2021 |
| JOHNVIAN NYAMSISA | GM-TREASURY | SIGNED | 10-07-2021 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 10-07-2021 |

216354502

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD, DOLPHIN** GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD, ROCK CITY TAKERS AUCTION MART kwa niaba ya Access Microfinance Bank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | ISOHE/MWITA,CHRISTOPHER | ISOHE/MWITA,CHRISTOPHER | NYUMBA | MBONDOLE | 28/07/2021 |
| 2 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | TEMRA/A,VALERY | TEMRA/A,VALERY | NYUMBA | MZINGA-KITUNDA | 28/7/2021 |
| 3 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MSANGI/HAMIS,ABEID | MSANGI/HAMIS,ABEID | KIWANJA | KISARAWE | 28/7/2021 |
| 4 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MOHAMED/O,ISMAIL | MOHAMED/O,ISMAIL | KIWANJA | CHATEMBO VIKINDU | 28/07/2021 |
| 5 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MKUMBA/A,SHAUN | MKUMBA/A,SHAUN | NYUMBA | MAJI MATITU | 06/08/2021 |
| 6 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | SEGANJA/MADUMA,DIANA | SEGANJA/MADUMA,DIANA | NYUMBA | PUGU | 11/08/2021 |
| 7 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | NDALI/K,BAKARI | NDALI/K,BAKARI | KIWANJA | KIBAMBA MKURANGA | 12/08/2021 |
| 8 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MASIKA/O,RAJABU | MASIKA/O,RAJABU | NYUMBA | KIZAPALA | 30/07/2021 |
| 9 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | TEGAMA/MBINGA,SOLOMONI | TEGAMA/MBINGA,SOLOMONI | NYUMBA | PUGU | 18/08/2021 |
| 10 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | MNONGA/LEMBA,WILFRED | MNONGA/LEMBA,WILFRED | KIWANJA | KILUNGULE | 19/08/2021 |
| 11 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | KANDOMYE/I,JUMA | KANDOMYE/I,JUMA | NYUMBA | MAPUNDA KIVULE | 29/07/2021 |
| 12 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | HASANI/ABDU,AMINA | HASANI/ABDU,AMINA | KIWANJA | KITONGA & MKEPO | 25/08/2021 |
| 13 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | BAWAZIR/H,AMNE | NDUNJE/S,JUMA | NYUMBA | KINGUGI | 29/07/2021 |
| 14 | TEMEKE | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | YANGWIKE/RASHID,FATUMA | KIMO/KASSIMU,MALIKI | NYUMBA | NZASA 'A' | 29/07/2021 |
| 15 | TEMEKE | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | MANGAO/HUSSEIN,HAMZA | MANGAO/HUSSEIN,HAMZA | KIWANJA | CHANIKA - LUKOONI | 30/07/2021 |
| 16 | TEMEKE | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD | KINAU/ALLY,SALUM | KINAU/ALLY,SALUM | KIWANJA | MBAGALA - SAKU | 30/07/2021 |
| 17 | TEMEKE | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD | SHABAANI,TATU | AKIDA/SAIDI,ALLIY | NYUMBA | YOMBO KIWALANI | 30/07/2021 |
| 18 | TEMEKE | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD | CHRISTOPHER,TABU | MALINZI/HERMANY,NARCIS | NYUMBA | YOMBO | 30/07/2021 |
| 19 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | BANDIO/L, GERMIN | BANDIO/L,GERMIN | HOUSE WITH ALTERNATIVE MORTGAGE | MKOLANI – MWANZA | 30/07/2021 |
| 20 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTIION MART | BENARD/L, BENARD | SANGIJA/ O, VERONICA | HOUSE WITH TITTLE NO. 52984 & TITTLE NO. 52937 | LUCHELELE- MWANZA | 30/07/2021 |
| 21 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | ESMAIL/ IQBAL, MOHAMED | NYANDA / MICHAEL, EMMANUEL | HOUSE WITH TITTLE NO. 51785 | NYEGEZI – MWANZA | 30/07/2021 |
| 22 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | LAKE SECURITY SERVICES | MUKAYU / J, EUSTACE | LAND WITH TITTLE NO. 29302 & TITTLE NO. 31560 | MISUNGWI – MWANZA | 28/07/2021 |
| 23 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | MADINDA / B, GABLIEL | MADINDA /B, GABLIEL | GODOWN WITH TITTLE NO. 43332 | NZEGA - TABORA | 28/07/2021 |
| 24 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | MASHAURI/ T, AMOS | MASHAURI/T, AMOS | LAND WITH TITTLE NO. 16095 & TITTLE NO. 40033 & LAND WITH ALTENATIVE MOARTGAGE | BWIRU & KABUHORO IBANDA MWANZA & ISAMILO – MWANZA | 28/07/2021 |
| 25 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | NYAKIHA/ PETER, BENARD | NYAKIHA/ PETER , BENARD | HOUSE WITH TITTLE NO. 64711 | GEITA | 30/07/2021 |
| 26 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | NYAMTABA / G, EDWIN | SINGU/ D, MALIYAHEWA, | GODOWN WITH TITTLE NO. 884 | TINDE | 29/07/2021 |
| 27 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | RWEKAKA SAID AND SONS COMPANY | RWEKAKA / S, SAID | LAND WITH TITTLE NO. 37843 | LUCHELELE – MWANZA | 28/07/2021 |
| 28 | PAMBA | ROCKY CITY TAKERS AUCTION MART | SINGU/ D, MALIYAHEWA | SINGU/ D, MALIYAHEWA | HOUSE & GODOWN WITH ALTENATIVE MORTGAGE | TINDE | 29/07/2021 |
| 29 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | ATHANAS/ C, KAIJI | ATHANAS /C, KAIJI | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | GEITA | 30/07/2021 |
| 30 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | KYARUZI /G, GRATION | KYARUZI/ G, GRATION | LAND WITH TITTLE NO. 53359 | BUSWELU – MWANZA | 28/07/2021 |
| 31 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | KAPOSWE/ I, SHABANI | KAPOSWE /I, SHABANI | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | MAHINA – MWANZA | 28/07/2021 |
| 32 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | MGEMA/ O, PHILIPO | MGEAMA/ O, PHILIPO | HOUSE WITH ALTENATIVE MOARGAGE | MWAHILI – MWANZA | 28/07/2021 |
| 33 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | MGIDANGE /W, GRAYSON | MGIDANGE /W, GRAYSON | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | MABATGINI ISENI - MWANZA | 28/07/2021 |
| 34 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | MPANGA /W, JOHN | MPANGA /W, JOHN | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | MAGU | 28/07/2021 |
| 35 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | MUSHI /E, LAURENCE | MUSHI /E, LAURENCE | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | NYASAKA MSUMBIJI-MWANZA | 28/07/2021 |
| 36 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | NELIS ENGLISH MEDIUM SCHOOL LIMITED | NELIS ENGLISH MEDIUM SCHOOL LIMITED | LAND WITH ALTENATIVE MORTGAGE | MKOLANI – MWANZA | 28/07/2021 |
| 37 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | SHIJA/ P, BONIFACE | NSUMBA / Z, ALOYCE | HOUSE WITH TITTLE NO. 20001 | NYAKATO – MWANZA | 28/07/2021 |
| 38 | PAMBA | DOLPHIN AUCTION MART | ABDALLA /MUSA, SHAMSI | ABDALLA / MUSA , SHAMSI | LAND WITH ALTENATIVE MORTGAGE | IGOMA – MWANZA | 29/07/2021 |
| 39 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | DOMICIAN /D, AUDAX | DOMICIAN /D, AUDAX | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | NYASAKA - MWANZA | 29/07/2021 |
| 40 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | KIMARO / ELIASHISA, ALPHAYO | KIMARO / ELIASHISA, ALPHAYO | HOUSE WITH ALTENATIVE MORTGAGE | MWINUKO KITANGIRI – MWANZA | 29/07/2021 |
| 41 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | NG'WAHWA /JULIUS , PASCHAL | FAUSTINE / FRANKY, FRANCO | HOUSE WITH TITTLE NO. 30638 | KISEKE – MWANZA | 29/07/2021 |
| 42 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | SHIJA/ KIPEJA, LEONARD | SHIJA/ KIPEJA, LEONARD | HOUSE WITH TITTLE NO. 53719 | IGOMA – MWANZA | 29/07/2021 |
| 43 | PAMBA | NUTMEG AUCTIONEERS &PROPERTY MANAGERS CO.LTD | KATARAMA /SIMON, STRATON | SAMWEL /S, NEEMA | HOUSE WITH TITTLE NO. 53947 | BWIRU – MWANZA | 29/07/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzangatiwa
4. Muda ni kuanzia saa 4.30 Asubuhi

**MAWASILIANO**
**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD - 0754497396**
**MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED - 0755506970**
**DOLPHIN GENERAL BUSINESS INTERPRISES C. LTD - 0754448694**
**ROCK CITY TAKERS AUCTION MART - 0713342969**
**WOTE MNAKARIBISHWA**


# Wafukua kaburi, waondoka na viungo vya marehemu

**Na Renatus Masuguliko**, MAGU

WAKAZI wa Kijiji cha Kitongo na vijiji jirani vya kata ya Sukuma, wilayani Magu, mkoani Mwanza wamekumbwa na taharuki baada ya watu wasiojulikana kuvunja kaburi la mtoto na kutoweka na baadhi ya viungo vya marehemu ikiwamo kichwa, miguu, uti wa mgongo na mikono. Tukio hilo linahusishwa na imani za kishirikina.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'azi, alisema uchunguzi umeanza na asingependa kulizungumzia zaidi ili kuepuka kuvuruga upelelezi.

"Ni kweli tukio hilo limetokea na tayari askari wamefika eneo hilo na wengine bado wapo eneo la tukio kwa uchunguzi...ninachowaomba wananchi wa Wilaya ya Magu na Mkoa wa Mwanza wasiwe na hofu na pia watoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi wakati likifanya upelelezi wake," alisisitiza.

Akizungumzia tukio hilo, bibi wa marehemu, Daines Maige, alisema mjukuu wake alikuwa wa jinsi ya kike mwenye umri wa miezi 20 na alifariki dunia mwaka jana.

Alisema kaburi la marehemu lilifukuliwa na watu wasiojulikana na kutokomea na baadhi ya viungo vya mwili wake.

Pia alisema watu hao baada ya kukamilisha kitendo hicho waliacha nyundo inayodaiwa kutumika kubomoa kaburi hilo.

Alisema baada ya askari polisi kupata taarifa walifika siku iliyofuata eneo la tukio na kushiriki kusimamia ufukuaji wa kaburi hilo.

Polisi waligundua baadhi ya viungo vilikuwa vimechukuliwa ikiwamo fuvu la kichwa, mikono, miguu na uti wa mgongo.

Mmoja wa wanakijiji, Revocatus Ngusa, alisema yupo tayari kushirikiana na polisi ili kukomesha vitendo hivyo vya kikatili.

Kwa upande wake, Heneriko Limbe, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitongo B, alisema kitendo cha polisi kufika mapema kijijini hapo kimesaidia kupunguza hasira za wananchi waliokerwa na ukatili huo.

Alisema wananchi walikuwa na hasira hali ambayo ingesababisha mauaji kwa watu waliokuwa wakiwashuku.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Posta (TPB), Sabasaba Mushingi, akiongoza kikao kati ya benki yake na uongozi wa Shirika lisilo la kiserikali la Social Action Trust Fund (SaTF) kwa ajili ya kuhitimisha mradi wa 'Diginitizing Information Saving Mechanism, Master Card Foundation', mkutano huo ulifanyika ofisini kwake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Kortini madai ya kusafirisha kilo 1 ya heroine

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na shtaka la kusafirisha kilo 1.02 ya dawa za kulevya aina ya heroine.

Washtakiwa hao wametajwa kuwa ni George Mwakang'ata, Andrew Paul na Said Mgoha, wote wakazi wa jijini Dar es Salaam.

Walisomewa shtaka lao katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritha Tarimo.

Wakili wa Serikali, Yusuph Abood, alidai kuwa Juni 21, mwaka huu, eneo la Mivinjeni Wilaya ya Temeke, washtakiwa walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Hakimu alisema washtakiwa warudishwe mahabusu mpaka Julai 27, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa tena.

# Mwili watupwa nyuma ya msikiti ukiwa utupu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Majengo, Manispaa ya Shinyanga, Lucia Michael maarufu mama Kulwa, amekutwa ameuawa na watu wasiojulikana na mwili wake kutupwa nyuma ya msikiti.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana na uligunduliwa na majirani majira ya saa 12 asubuhi baada ya kuuona mwili huo ambao hakuwa na nguo.

Akielezea tukio hilo mmoja wa majirani hao, Anastazia Amosi, alisema baada ya kupata taarifa, alifika eneo la tukio na kumkuta jirani yake akiwa ameuawa na mwili wake ukiwa mtupu na kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa mtaa.

"Mwanamke huyu ni jirani yetu ana watoto watatu na kazi yake ni msusi maarufu sana hapa mtaani kwetu, tunasikitika sana kumkuta akiwa ameuawa tena kavuliwa nguo zote," alisema Amosi.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Majengo, Iddi Bwana, alisema mwanamke huyo huenda aliuawa na vibaka kwa sababu walianza kupambana vichochoro na kisha mwili wake kutupwa nyuma ya msikiti jirani na makazi ya watu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha mauaji hayo.



Wananchi wa Majengo Manispaa ya Shinyanga, wakiangalia mwili wa mwanamke Lucia Michael maarufu Mama Kulwa, ambaye ameuawa na watu wasiojulikana usiku jana, nyuma ya Msikiti wa Majengo, mwili huo ulikutwa ukiwa utupu. **Picha: MARCO MADUHU**

# Ummy ataka wadau kuwekeza rasilimali watu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amewataka wadau wa maendeleo kuwekeza katika rasilimali watu ili kupata watumishi wenye weledi katika kutoa huduma bora ya afya kwa jamii.

Waziri Ummy alitoa wito huo jana wilayani Kasulu mkoani Kigoma baada ya kupokea vifaa tiba katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu vilivyotolewa na Benki ya Maendeleo TIB kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Kasulu.

Alisema kwa sasa kipaumbele cha serikali ni miradi inayogusa maisha ya wananchi hasa katika seka za afya, miundombunu, elimu na maji katika ngazi ya msingi.

"Tunawasihi wadau wote wa maendeleo nchini kuelekeza nguvu zao katika kuwekeza kwenye miradi inayowalenga moja kwa moja wananchi badala ya kutenga bajeti kubwa kwa ajili ya mafunzo na semina," alisema.

Waziri Ummy aliongeza kuwa wadau wengi wa afya wamekuwa wakiwekeza katika semina na mikutano na kusahau kuwa vifaa vinavyoletwa kwa ajili ya kutolea huduma vinahitaji kuwa na wataalamu ambao wanauwezo wa kuvitumia.

Aliwataka viongozi wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanapokaa na wadau wa maendeleo wahakikishe wanatoa vipaumbele vitakavyosaidia kuleta mabadiliko katika sekta ya afya na elimu.

Aliishukuru benki hiyo kwa kuunga mkono juhudi za serikali za kuimarisha huduma za afya ya msingi kwa kutoa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 12.

Meneja Masoko na Uhusiano wa TIB, Saidi Mkabakuli, alisema benki imetoa msaada huo kwa kutambua ukweli kuwa sekta ya afya ni mojawapo ya eneo la kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo.

"Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya afya, TIB kama benki inayotekeleza vipaumbele vya serikali, tuliona ni vyema kuchangia baadhi ya vifaa tiba kwa ajili ya hospitali ya wilaya ya Kasulu kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali za kuimarisha huduma za afya ya msingi katika mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema.

Alisema msaada huo unalenga kusaidia mpango mkakati wa TAMISEMI ambao unatekeleza malengo mahsusi kama vile kuimarisha na kuhakikisha vituo vya kutolea huduma vilivyokamilika vinaanza kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba.

# Tahadhari dhidi ya corona yashauriwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Luteni Josephine Paul Mwambashi, amewataka wananchi wa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona, ambao umerejea kwa kasi awamu ya tatu.

Luteni Mwambashi alitoa kauli hiyo jana wakati akitoa ujumbe wa mbio za Mwenge, baada ya kuweka jiwe la msingi katika Shule ya Sekondari Mwakata, ujenzi uliogharimu Sh. milioni 137 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Msalala pamoja na nguvu za wananchi wa kata hiyo.

Alisema, Mwenge wa Uhuru unakwenda sambamba na uchukuaji tahadhari dhidi ya corona, na kwamba kila mmoja anatakiwa kuchukua tahadhari bila kusukumwa na viongozi.

Alisema asiyevaa barakoa hataruhusiwa kushiriki kaatika shughuli za mbio za Mwenge wa Uhuru.

Aliitaka Wizara ya Afya iendelee kutoa maelekezo bora ya namna ya kujikinga, na kwamba kila mmoja atakiwa kuzingatia maelekezo hayo.

# TAWA: Anzisheni mashamba ranchi

**Na Christina Haule**

KAIMU Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mabula Nyanda Misungwi, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kuanzisha mashamba, ranchi, bustani za wanyamapori ili waweze kujiongezea kipato.

Misungwi alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) mkoani Dar es Salaam.

Alisema wananchi wanapaswa kuchangamkia kuanzisha mashamba ya wanyamapori, kwani kutawasaidia kujiongeza kipato kutokana na ongezeko la uhitaji wa nyamapori unaotokana na uanzishwaji wa mabucha nchini.

Aidha, Kamanda Misungwi aliwataka wananchi kuitumia vyema fursa iliyotolewa na serikali ya uanzishaji wa mabucha ya nyamapori, na kwamba hiyo itasaidia kupatikana kwa nyamapori mapema pale inapohitajika.

# Wafurika banda la RITA kufuatilia vyeti vya kuzaliwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini(RITA), umelazimika kuwatumia vijana maalum wa ulinzi walio chini ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania(TANTRADE), ili kusaidia kutoa baadhi ya huduma ndogo kwa umati wa wananchi wanaofika katika banda hilo kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) kwa ajili kuhitaji huduma.

Banda la RITA ni miongoni mwa ambayo yamekuwa yakifurika watu tangu maonyesho hayo yaanze Juni 28, mwaka huu.

Kwa mujibu wa uongozi wa wakala huyo, wengi wanaofika katika banda hilo ni wale wanaofuatilia vyeti vya kuzaliwa.

Akizungumza na Nipashe kwenye banda lao, Ofisa Habari wa RITA, Edwin Mbekenga, alisema wamelazimika kutumia vijana hao wa ulinzi kuongeza nguvu ya ulinzi kutokana na umati unaojitokeza pamoja na kusaidia kazi ndogo ndogo ikiwamo kuwaelekeza watu hao namna ya kuchukua tahadhari dhidi ya maambukuzi ya ugonjwa wa corona. "Tumelazimika kuwatumia vijana hawa ili watusaidie kuimarisha ulinzi kwa sababu idadi ya watu imekuwa kubwa mno na kama unavyofahamu sasa hivi kuna mlipuko wa ugonjwa wa corona na hatuwezi kuwaacha hivi hivi maana itakuwa ni hatari, kwa hiyo hawa vijana tumewapatia malekezo ya kuwahakikishia hawa watu usalama wao, na namna ya kuwapatia maelekezo ya kujikinga na ugonjwa huu," alisema Edwin.

"Si tu kwamba tumelazimika kuongeza hawa vijana wa ulinzi, lakini hata kwa upande wa watumishi, imebidi tuongeze timu nyingine tofauti na ile tuliyoanza nayo mwanzoni mwa maonyesho kwa sababu kadri siku zinavyosogea na idadi ya watu wanaokuja kufuata huduma ya RITA kwenye maonyesho haya nayo imezidi kuwa kubwa."

Edwin alisema kutokana na wimbi kubwa la watu wanaojitokeza kwenye banda lao, wanalazimika kutoa huduma hadi usiku.

"Muda wa kufunga mabanda humu ni saa 12 jioni, lakini sisi tunalazimika kutoa huduma hadi usiku, inatubidi tufanye hivyo kwa sababu hatuwezi kuwarudisha watu bila kuwahudumia na wanatumia kiingilio kuja huku, kwa hiyo idadi yoyote inayojitokeza kujiandikisha kila siku lazima tunahakikisha kwamba wote wamepatiwa huduma," alisema Edwin.

Alisema mpaka sasa watu waliojiandikisha na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa katika maonyesho hayo ni zaidi ya 6,000.

Alitoa ushauri kwa wananchi wasipende kusubiri vipindi vya matukio kama hayo ya maonyesho ndio washughulikie vyeti vyao, kwa kuwa huduma hizo hutolewa kila siku katika ofisi za RITA.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, akiwajulia hali wagonjwa wa corona, ambao wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, huku akitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi wa mkoa huo, kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri: W'biashara eleweni mfumo kidigitali

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabaan, amesema kuna umuhimu kwa wafanyabiashara kuwa na uelewa wa namna ya kutumia mfumo wa kidijitali kupata taarifa mbalimbali za kibiashara.

Alisema tayari mfumo huo umewekwa ili kumrahisishia mfanyabiashara kupata taarifa sahihi na kuendesha shughuli zake kwa urahisi zaidi.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa mfumo wa taarifa za biashara kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya 45 ya Biashara Dar es Salaam (DITF), waziri huyo alisema wanaamini mfumo huo utasaidia kuondoa changamoto za kukosa taarifa za kibiashara zilizokuwa zikiwakabili wafanyabiashara hao na pia utaleta tija katika uendeshaji wa shughuli zao.

Pia alisema mfumo huo utasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa urasimu uliokuwapo awali. Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliwataka wafanyabiashara kwenda na wakati na kufanya kazi kisasa kwa kutumia njia ya mtandao.

Alisema biashara kwa njia ya mtandao inasaidia kurahisisha muda na hata kupata wateja wengi tofauti na njia ilivyozoeleka.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), Balozi Mteule, Edwin Rutagaruka, alisema wanaamini mfumo huo utaleta tija katika sekta hiyo na kwamba watahakikisha wanausimamia kwa utaalamu mkubwa ili ulete manufaa ya kiuchumi kwa wafanyabiashara wenyewe na kwa nchi.

## Wapewa ushauri kulima kibiashara

**Na Elizabeth Zaya**

WAKULIMA wameshauriwa kukitumia kilimo kubadili maisha yao kiuchumi badala ya kukitumia kwa ajili ya chakula pekee.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Mkuu wa Kampuni inayojishughulisha na kuwaunganisha wakulima kufanya kilimo biashara (JATU), Mohammed Simbano, kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba.

Alisema kuna haja ya kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kote nchini ili wafanye shughuli za kilimo kwa kisasa ikiwamo kuwa na dhana bora za kulimia na kuvunia ambazo zitachangia kupata mazao mengi na kuyauza kwenye viwanda vikubwa.

"Kwenye sekta ya kilimo bado kuna tatizo, wakulima wengi bado hawajafikiwa kuwapatiwa elimu na kupata uwezeshaji wa kuingia katika kilimo cha kisasa, wapo ambao wanalima kwa mikono, wanahitaji kushikwa mkono," alisema Simbano.

"Ndio maana sisi JATU tuliamua kwenda kujikita huko kulisaidia kundi hili katika baadhi ya mikoa kuwaweka katika mfumo ambao utawasaidia kufikia kwenye kilimo hicho cha kisasa, kuhakikisha wanapata zana bora pamoja na masoko."

## Shule yataka hamasa ya umuhimu wa elimu

**Na Elizabeth Zaya**

UONGOZI wa shule za Scolastica zilizopo Himo mkoani Kilimanjaro umewahamasisha wamiliki wa shule na wadau wengine wa elimu kutumia fursa ya Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam(DITF) ambayo hufanyika kila mwaka, kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa elimu.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Masoko wa shule hizo, Johnson Msuya, kwenye banda lao lililopo katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam ambayo yanatarajiwa kufungwa leo.

Msuya alisema wamegundua kwamba hakuna mwitikio wa kuridhisha kwa wamiliki na wadau wengi wa shule hususani za msingi na sekondari katika kushiriki kwenye maonyesho hayo.

"Mpaka tukahisi kwamba labda washiriki kutoka kwenye upande wa shule ni Scolastica pekee japo bado tunajipa matumaini kwamba labda katika siku hizi mbili zilizobaki tutabahatisha kuona mdau mwenzetu hata mmoja, kwa sababu fursa za maonyesho kama hizi ndizo zinatusaidia kutukutanisha na kubadilishana mawazo."

Alisema miongoni mwa vitu vilivyousukuma uongozi wa shule za Scolastica kushiriki katika maonyesho hayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanaendelea kutoa elimu kwa Watanzania hususani wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa kuwapatia elimu bora watoto wao pamoja na kutoa elimu ya namna ya kumsaidia mwanafunzi kuchagua na kufikia malengo ya taaluma ya ndoto yake.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 13, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Wanakijiji 300 walivyojiongeza wajenga shule sekondari, msingi



Ukurasa 13

Ni zama za kufuatilia ubora, usalama wa kila kinacholiwa



Ukurasa 14

## Wanacholenga TPDC, vituo vya mafuta

TEKNOLOJIA

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Wenye ulemavu wanavyoshangaza kiufundi

## • Ni kusuka mashine, samani kiufanisi zaidi

"KWANGU kuishi na ulemavu sichukulii kama changamato bali naona fursa tena ni zawadi." Ni ushuhuda wa ujasiri kutoka kwa Mohamed Selemani mwenye ulemavu wa usonji (autism), wakati akifurahia kutengeneza samani za ndani na kuunda mashine mbalimbali.

Anayasema hayo wakati anazungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa ameishi na usonji kwa miaka 28, lakini si kikwazo kwa vile anasoma elimu ya ufundi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) Dar es Salaam.

Elimu hiyo imemwezesha kutengeneza vifaa mbalimbali na kuunda mashine lakini ana kipaji cha kuelewa na kushika vitu kwa kasi anapofundishwa darasani.

Akiwa na uso wa furaha kwenye banda la VETA wakati wa Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Dar es Salaam - Sabasaba, Mohamed, anasema: "Namshukuru sana baba yangu mkubwa kwa kunilipia ada nikasoma elimu ya ufundi VETA hadi kufika hapa nilipo leo."

"Alichukua hatua baada ya kuona ninapata shida na kuishi maisha magumu baada ya bibi yangu mlezi kufariki na hatimaye nikatumbukia kwenye shida na umaskini."

Anasema kupitia mafunzo ya ufundi anatengeneza majiko mbalimbali ya chuma yanayotumia mkaa na mashine mbalimbali zinazotumia umeme kuranda mbao.

Aidha, ameunda mashine ya kubangua karanga inayoweza kutumiwa na wajasiriamali mijini na vijijini badala ya mikono kubangua karanga.

**KILICHOMSUKUMA KUSOMA**

Anasema ni baada ya kupata shida, kukosa chakula kufuatia kifo cha bibi yake. Lakini zaidi ni hamu ya kuujua ufundi ili aweze kujitegemea kwa kutengeneza bidhaa zinazomwongezea kipato ili kumudu maisha yake na kuondokana na utegemezi.

"Nilipoanza kusoma VETA Chang'ombe nilijisikia safi, niliona kuwa nitaweza kutengeneza vitu mbalimbali kwa sababu nina kipaji cha kushika mapema vile ninavyofundishwa. Leo nina miaka mitano chuoni nikisoma kozi ya uungaji na utengenezaji bidhaa za vyuma." Anaongeza Mohamed.

AKiwa kwenye banda la VETA Sabasaba, anasema: "Nimekuja kwenye maonyesho kuwaonyesha walezi na wazazi pamoja na jamii kuwa siyo muda wa kuwaficha ndani watoto wenye ulemavu. Wawapeleke shuleni na vyuo vya VETA. Tena tunataka kuonyesha kuwa ukimsomesha mwenye mahitaji maalumu anaweza kubadilika na akazalisha bidhaa na hata kuajiri wengine."

Anaongeza kuwa wanataka kuihamasisha jamii kuwatambua wenye ulemavu na kuwachukua kwenye maeneo mbalimbali ya uzalishaji mfano, viwandani, karakana na ofisini.

**HISTORIA YA MOHAMED**

Licha ya kuongea kwa msaada wa mwalimu wake Kintu Kiranga, anasema amelelewa na bibi yake waliyekuwa wakiishi Majohe Wilaya ya Ilala na kwamba mlezi huyo alikuwa akilima mpunga ili kupata chakula, akimtunza na ndiye aliyemsomesha katika Shule ya Msingi Ukonga. Alipomaliza darasa la saba 2012, aliendelea kulima mpunga na bibi yake ambaye alifariki mwaka 2015, na kubakia bila msaada hali iliyomlazimisha kuzurura mitaani kwa vile maisha yalikuwa magumu sana.

"Nilikuwa nazoa taka nyumbani kwa watu mbalimbali kwa ujira kidogo. Pia nilikuwa nauza maji vyote viwili vikinipatia Shilingi 5,000 kwa siku. Nilifanya haya kwa miaka miwili hata hivyo nilishindwa maisha yalizidi kuwa magumu," anasema.

Aliona hakuna mafanikio ila kumwomba baba yake mkubwa, amsomeshe VETA naye akakubali na leo amefikia hatua hiyo ya kuwa fundi bora.

"Namshukuru baba mkubwa na mwalimu Kiranga, bila msaada wao pengine nisingeweza kufika hapa."



Paulo Ngunyari akiwa kazini Sabasaba kutengeneza samani kwa kutumia mashine aliyoiunda. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

**WENYE ULEMAVU TUNAWEZA**

Anasema Paulo Ngunyari (31), mshiriki mwingine kwenye Maonyesho ya Sabasaba ndani ya banda la VETA, anayeishi na ulemavu wa viungo. Ni kozi ya uungaji vyuma na utengenezaji wa bidhaa za vyuma (welding fabrication) na mwenye ujuzi wa kutengeneza majiko ya chuma, majalo (vijiko vya kuchotea mkaa na moto), kushirikiana na mwalimu kutengeneza mashine mbalimbali kama vile za kusaga juisi ya miwa na za kukatia mihogo.

"Ninafanya kazi hii kwa ufanisi na wateja wanafika chuoni kuweka oda na tunawatengenezea wanachohitaji."

Anasema anashiriki Sabasaba kuonyesha jamii kuwa inawezekana wenye mahitaji maalumu wakipata mafunzo ya ufundi na wakajikwamua kimaisha na kuwataka kwanza wajikubali kwamba wanaweza.

Ushauri wa Ngunyari kwa wenye ulemavu ni kuwahimiza kwanza wajikubali walivyo na kujiamini kuwa wanaweza na waende kwenye vyuo vya VETA au shuleni kujifunza.

**KINACHOWAUMIZA**

Ngunyari anawanyooshea kidole mawaziri, watendaji serikalini na wabunge kuwasahau na kila wakati kutembelea vyuo vingine vyenye wanafunzi walio na viungo timilifu.

"Watoa maamuzi hawatutembelei ndiyo maana tumekuja hapa ili waje watuone kwa sababu watoto wa aina hii wakifundishwa wanawaweza kuleta mabadiliko na kujitegemea kimaisha."

Wahitaji hao Mohamed na Ngun-

INAENDELEA UK.12

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Wanakijiji 300 walivyojiongeza wajenga shule sekondari, msingi



Madarasa ya Shule ya Msingi Nyasaungu mkoani Mara yanayojengwa kwa nguvu za wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

BAADHI ya wanavijiji wanaotambua umuhimu wa elimu wanafanya kila jitihada ili kufanikisha masomo ya watoto wao katika mazingira rafiki na salama.

Miongoni mwa hao wanaojiongeza ni wanakijiji cha Nyasaungu wanaoishi wilayani Musoma mkoa wa Mara.

Azma yao ni kuona shule inakuwa mahali pazuri pa wanafunzi kujifunzia na kufundishiwa, lakini pia wanafunzi wasitembee umbali mrefu kufuata elimu.

Kwa kuona umuhimu wa elimu, wakazi hao wameamua kujenga sekondari ya kijiji hicho ili kuwapunguzia watoto wao kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

Si ujenzi wa sekondari tu, bali pia kwa sasa wanashirikiana kujenga madarasa ya Shule ya Msingi Nyasaungu ili kuzuia watoto kusomea chini ya miti kwa kuwa mazingira hayo si rafiki katika elimu. Mwenyekiti wa kijiji hicho, Magesa Marera, akizungumza na Nipashe kuhusu juhudi hizo anasema, ujenzi wa sekondari ya kijiji unaendelea, lakini wa madarasa mapya kwa ajili ya shule ya msingi nao pia unafanyika.

"Tunajenga sekondari ya kijiji ili kuwapunguzia watoto safari ndefu wasitembee umbali mrefu kufuata elimu, lakini tunajenga madarasa mapya ya shule ya msingi ili watoto wasirundikane au kusomea chini ya miti," anasema Marera.

Mwenyekiti huyo anasema, ujenzi wa sekondari ulianza mwaka 2019 na kwamba hadi sasa madarasa 78 yameshajengwa, huku maboma mapya 25 yakiwa katika hatua za mwisho kukamilika ili baadaye shule ianze kazi.

"Ujenzi wa sekondari ulianza baada ya wananchi kuamua kwa pamoja kwamba wanataka sekondari ya kijiji chao, ili kuwapunguzia watoto wao kutembea umbali mrefu kufuata elimu sekondari ya kata nyingine," anasema.

Marera anafafanua jinsi wanakijiji walivyochangia ujenzi na kwamba, kaya zenye ng'ombe zaidi ya 100, zilikubali kuchangia zaidi ya Sh. 200,000 na zenye ng'ombe kati ya 50 hadi 99, michango yao ni Sh. 100,000.

"Kaya zenye ng'ombe chini ya 50, michango yao ni Sh. 40,000, lakini pia nguvukazi za wananchi zinatumika kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji kwa ajili ya ujenzi huo," anasema.

Anasema, kijiji hicho kina vitongoji vitano na wakazi 315, ambao wameungana kuhakikisha wanaboresha huduma za elimu katika kijiji chao ikiwamo kujenga sekondari ya kijiji na kuongeza madarasa ya shule ya msingi.

Kaimu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyasaungu, Stephen Musiba, anasema, shule hiyo ilianzishwa mwaka 1999 na kwa sasa ina wanafunzi 788 na madarasa nane na wanahitaji 14.

"Darasa la tatu ndilo lenye mrundikano mkubwa wa wanafunzi darasani, ambapo 131 wanasomea chumba kimoja, hali ambayo imewalazimu wazazi kuungana na serikali katika ujenzi wa madarasa mapya," anasema Musiba.

Mbali na uhaba wa madarasa, shule hiyo pia ina matundu nane ya vyoo huku mahitaji ni 39 na kwamba zinahitajika pia nyumba 15 za walimu, lakini zilizopo ni tano.

"Wananchi wanaendelea kuchangia kwa hali na mali katika kuboresha mazingira ya shule yao ambapo kila kitongaji Sh. 107,000 na matofali 40 kwa kila awamu ya ujenzi," anasema.

Anaongeza kuwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), imechangia Sh. milioni 12 kwa ajili ya kupua darasa na ofisi moja ya walimu, huku Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (PCI) likijenga matundu nane ya vyoo na linachimba kisima cha maji.

Anasema Mbunge Profesa Sospeter Muhongo, kupitia mfuko wa jimbo akichangia mifuko 50 ya saruji, madawati 130, vitabu zaidi 1,000 na mabati 108.

### MAELEZO YA DED

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Musoma, John Kayombo, akitoa rai yake anasema wanavijiji wanatakiwa kuendeleza moyo wa kujitolea kwenye maeneo yao ili kuboresha elimu kwa manufaa ya watoto wao.

Anasema, katika wilaya hiyo, wapo baadhi ya wananchi katika vijiji mbalimbali ambao wanaendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu kwa kujitolea kuchangia nguvukazi.

"Wakazi wa Nyasaungu ni miongoni mwao, ambao wameamua kujenga shule ya sekondari, lakini mbali na hilo, wanashiriki kuboresha miundombinu katika shule ya msingi ya kijiji hicho," anasema Kayombo.

Hatua hiyo imeonyesha ni jinsi gani wanavyotambua umuhimu wa elimu kwa ajili ya watoto wao na kwamba halmashauri yake inawatia moyo waendelee kuunga mkono na kuhamasisha wengine kuchukua hatua kama hizo, anasema Kayombo.

# WENYE ULEMAVU WANAVYOSHANGAZA KIUFUNDI

INATOKA UK.11

yari wanawaomba viongozi wawapatie maeneo ya kufanyia kazi za ufundi, vitendea kazi za ufundi na maeneo ya kuuza bidhaa zao kwa bei inayolipa gharama za kazi walizofanya.

"Wakati naanza kusoma nilijisikia vizuri na niliona kama nitaweza kusoma na kutengeneza vitu mbalimbali kwa sababu nilikuwa na kipaji cha kushika mapema ingawa nilikuwa na ulemavu wa usonji na sasa hivi nina muda wa miaka mitano ninasoma 'course' ya uungaji na utengenezaji wa bidhaa za vyuma," anasema.

### KUINUA WAHITAJI

Mwalimu wa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na viungo, Kintu Kiranga, anasema wenye mahitaji maalumu wanafundishika na amewafundisha wanafunzi 11 wakiwamo 13 wenye ulemavu wa akili.

"Kazi hii ni muhimu kuwasaidia wahitaji, naiomba serikali iandae walimu wa ufundi wa kufundisha watu wenye mahitaji maalumu, kwa sababu tulioko ni wachache mno na wengi wamezeeka na wanastaafu kila uchao."

Kiranga anaeleza kuwa tangu alipohitimu mwaka 1980 katika Chuo cha Ufundi Chang'ombe mpaka leo yuko peke yake na hakuna mwalimu mwingine licha ya kwamba anazeeka na anakaribia kustaafu. Anaishauri iwekeze zaidi kusomesha na kuandaa walimu wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalumu na pia jamii ikubali kuwaajiri wahitimu wa mafunzo ya ufundi wenye mahitaji maalumu lakini pia wanunua bidhaa zao na kuwapa kazi za kuwatengenezea pale wanapojiajiri.

"Wenye viwanda, wajasiriamali wanaofungua viwanda vidogo wawajiri vijana hawa kwa sababu wana uwezo na ujuzi wa kufanyakazi kama watu wengine." Anasema Mwalimu Kiranga.

### ANACHOWAFUNDISHA VETA

Mwalimu Kiranga anasema wenye mahitaji hufundishwa kuunga, kutengeneza bidhaa za vyuma, ubunifu wa vifaa mbalimbali kulingana na ulemavu walio nao na mpaka sasa wamefanikiwa kujitegemea na baadhi wanaoishi wenyewe kutokana na kipato wanachopata.

Anawaalika wateja kuja kwenye karakana ya VETA kununua mashine na samani mbalimbali ili kuunga mkono juhudi za kuendeleza teknolojia na kuinua maisha wenye mahitaji maalumu.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ni zama za kufuatilia ubora, usalama wa kila kinacholiwa

KINAPOTAJWA chakula ni suala linamhusu kila mmoja anayeishi bila kujali utajiri, umaskini wala utaifa, kwa vile kila mtu anahitaji kupata mlo bora wenye lishe na ulio salama ili aishi.

Ndiyo sababu Umoja wa Mataifa (UN), Septemba mwaka huu, unaitisha mkutano wa kilele kujadili na kutoa mwelekeo wa suala la upatikanaji wa chakula bora na salama kwa wote.

UN inaamini kuwa chakula kina mchango mkubwa kufanikisha kufikiwa malengo 17 endelevu ya umoja huo na kuagiza kuiangalia upya mifumo ya chakula.

Katika kutekeleza juhudi hizo, Wizara ya Kilimo na wadau wa mwamvuli unaonganisha mashirika ya kiraia yanayoshughulika kilimo (ANSAF) wanakutana jijini Dodoma kuangalia vipaumbele vya kuboresha mifumo hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF Audax Rukonge, anasema mifumo ya chakula inahusisha mchakato mzima wa kuzalisha, kukivuna, kukisafirisha, kukisindika hadi kinapoliwa mezani.

Anawaambia washiriki wa Mjadala wa Kitaifa wa Mifumo ya Chakula kuwa taifa linahitaji mifumo ya chakula endelevu inayozalisha chakula usalama na chenye virutubisho vya kutosha.

Aidha, anasema mifumo hiyo endelevu izingatie usalama wa chakula na ulinzi wa mazingira, utunzaji wa rasilimali kama maji, misitu, hewa na ardhi.

"Mifumo endelevu inahusisha ustawi wa wazalishaji wakulima, wasafirishaji, wasindikaji hadi walaji mezani," anasema Rukonge.

Anakumbusha mifumo hiyo kuwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, wavuvi, wasafirishaji, viwanda wasindikaji, wahifadhi wauzaji sokoni hadi chakula kinapofika mezani kuliwa.

Anazitaka asasi za kirai zinazojihusisha na kilimo kushughulika na usalama wa mifumo hiyo, kuanzia uzalishaji mashambani, majini, usafirishaji, usindikaji viwandani, uuzaji hadi kumfikia mlaji ili kiwe na ubora na usalama kwani katika kila hatua chakula kinaweza kuchafuliwa na kutishia afya.

Meya wa Dodoma, Profesa Davis Mwamfupe, anazungumzia kuboresha mifumo ya chakula, akisema ni muhimu iwe inayozalisha chakula cha bei nafuu wanayomudu watu wote bila kuwaacha wengine na njaa hasa wenye kipato kidogo.




Meya wa Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, akizungumzia mifumo salama ya chakula na wadau wa ANSAF jijini humo.

"Ili mifumo ya chakula iwe endelevu zaidi ituletee chakula salama na cha kutosha chenye lishe bora kwa wote. Isiwe ni mfugaji amedhoofika, mifugo imekonda haina maji, nyasi wala maeneo ya malisho."

Profesa Mwamfupe, anasema moja ya ajenda za kitaifa za kuwa na mifumo imara ya chakula ni kuhakikisha wakulima wanapata soko lenye bei zinazolipa gharama za uzalishaji ili wasipunjwe.

Anasema hayo yanawezekana kama kuna mijadala ya mara kwa mara ya kusikiliza wadau, kupokea mawazo na kuyafanyia kazi.

**CHAKULA HATARISHI**

Chakula ni maisha na usalama wake ni kipaumbele kinachotazamwa wakati wa mjadala wa mifumo endelevu.

Usalama wa chakula na ulaji vyakula hatarishi unaibuka karibu muda wote wa mjadala.

Wadau wana wasiwasi wa wananchi kula vyakula vinavyodhuru kutokana na mifumo ya uzalishaji kuingiliwa na teknolojia za viuatilifu na virutubishi visivyo salama.

Licha ya kutaka wananchi kula chakula salama kisichodhuru walaji na chenye ubora wanaonyesha hofu kuwa chakula kinapokosa usalama na ubora hugeuka kuwa sumu na kuchangia magonjwa yasiyoambukizwa.

Ofisa Kilimo Mkuu wa Wizara Kilimo, Margareth Natai, anasema iwapo chakula kitachafuka kwa mfano mahindi au nafaka zikichafuka na sumukuvu hakifai kwa binadamu wala mifugo.

Anasema: "Kama nafaka ina sumukuvu haifai kwa wanyama wala binadamu ni ya kuharibiwa mara moja. Haina tofauti na sumu inayotishia maisha."

Margaret anasema taifa linahitaji mifumo endelevu ya chakula ambayo itachangia kwenye usalama wa chakula na lishe bora kwa kila Mtanzania.

Mbunge wa Viti Maalumu (uwakilishi wa asasi za kiraia), Neema Rugangira, anamuunga mkono: "Usalama wa chakula uko shakani kutokana na matumizi makubwa yasiyo sahihi ya mbolea za viwandani, viuatilifu na dawa za kuhifadhia mazao, mambo yanayoathiri chakula kutokana na uwezekano wa kuchafuliwa na kemikali hizo."

Anaongeza kuwa usalama na ubora unahusisha jamii nzima ili kila mmoja atumie chakula salama na chenye virutubisho muhimu.

Akizungumzia kemikali anaonya kuhusu matumizi makubwa na kiholela ya mbolea, viuatilifu vya kuulia visumbufu na kuhifadhia mazao ambavyo vinachafua chakula na kutishia uhai wa walaji.

"Unakuta nyanya inamwagiliwa dawa leo na kesho iko sokoni... hata ng'ombe anachomwa sindano leo na kesho maziwa yanapelekwa sokoni. Hapo hakuna usalama wa chakula," anasema mbunge huyo.

Neema anasema mambo hayo yanahatarisha afya na huenda yanachangia ongezeko la magonjwa kama saratani na kwa ujumla maradhi mengi yasiyoambukizwa.

Anaikumbusha serikali kuiangalia upya Sera ya Taifa ya Lishe inayohitaji kuboreshwa na kwamba haijawahi kurekebishwa tangu ilipoanza kutumika mwaka 1993.

"Usalama wa chakula ni jambo muhimu mno linawagusa watu wote ndiyo maana nimefanikisha kushawishi bunge kuwa na kikundi cha wabunge vinara wa usalama wa chakula ili kuishahuri serikali na wadau wengine kwenye umuhimu wa kuhakikisha usalama na ubora wa chakula kwa Watanzania tunachokula."

Anaonya kuwa mazao, mbegu na mbolea za asili zinapotea na viatilifu asilia navyo vinasahaulika, akishauri kufanyika juhudi zaidi.

Wadau wanashauri wakulima, serikali na watafiti kuwezesha kuzalisha na kutunza mbegu za asili. Lakini Watanzania kula vyakula vya asili badala ya chips na vingine vya kukaangwa zaidi ambavyo asili yake si Tanzania.

**ATHARI ZA UTAMADUNI**

Akijadili kuhusu mifumo endelevu ya chakula, Stella Kimambo, kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la UN –FAO, anasema kuiga utamaduni wa kigeni kumeathiri mifumo ya ulaji na uzalishaji chakula nchini.

"Chakula huwaleta watu wote pamoja bila kujali umri wala jinsia hivyo ni jambo muhimu kujadili mifumo yake na kuendeleza ulaji ulio bora."

Stella anataja mambo yanayoathiri uzalishaji chakula na mifumo ya ulaji kama utamaduni. Mfano baadhi ya watu kuona kuwa ndizi, ugali au mhogo ndicho chakula 'supa' na hawataki kubadili fikira. Mtaalamu huyo, anaeleza kuwa

kuanzia sasa ni vyema kubadilika na kutumia lishe bora badala ya kula kimazoea na kutafuta utaalamu ufahamu zaidi wa vyakula na lishe bora.

Anasema wazazi, walezi na watoto wanapaswa kuzungumzia umuhimu wa chakula, usalama na ubora wake na kuwapa watoto elimu ya lishebora.

Anatoa mfano wa mtoto aliyehamaki na kushangaa kuona mti wa papai na matunda hayo yakiwa yameiva akashangaa na kuhoji kwanini hayoko ndani ya friji?

Stella anasema hilo linaonyesha kuwa kizazi cha sasa hakifahamu chakula, kinapozalishwa na namna ya kukipata.

**MAPENDEKEZO**

Washirika wanapendekeza serikali na wadau kuimarisha mifumo ya mbegu za asili na kuwa na benki ya mimea inayohifadhi mbegu na wanyama wa asili.

Aidha, wanapendekeza kutumia vyakula bora na vyenye lishe hasa vya asili.

Kutumia sheria, miongozo na teknolojia kusimamia uungizaji wa viuatilifu na virutubishi vyenye viwango ili kuepusha nchi kuwa jalala la kemikali za sumu za kilimo.

Aidha, wanashauri serikali kutoa miongozo ya bei na masoko mfano kwenye mifugo iuzwe kwa kupimwa uzito kwenye mizani badala ya kuangalia kwa macho.

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

# Wanacholenga TPDC, vituo vya mafuta

- Kuanzisha vituo kujaza magari gesi
- Injini mpya za CNG sasa ziko barabarani

ULINZI wa mazingira na kupunguza ongezeko la joto duniani ni suala linalofikirisha mataifa yote tena karibu kila sekta.

Injini za magari zinazotumia dizeli na petroli, zinatajwa kuchangia uchafu wa hewa na kuongeza hewa ukaa inayozidisha joto duniani, hivyo ili kuwa na injini na hewa safi, matumizi ya gesi na umeme kwenye magari badala ya mafuta yanapewa kipaumbele.

Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi wa Shirika la Maendeleo ya Petrol (TPDC), Dk. Wellington Hudson, anatoa maelezo ya matumizi ya nishati ya gesi kwenye magari katika mahojiano na Nipashe.

Anaanza kueleza gesi iitwayo CNG kuwa ndiyo inayotumiwa kwenye injini za magari, akifafanua zaidi anasema: "CNG ni kifupisho cha 'Compressed Natural Gas' ambayo ni gesi asilia iliyoshindiliwa katika mgandamizo mkubwa ili kuhifadhi kiasi kikubwa cha nishati hiyo kwenye chombo chenye ujazo mdogo ambayo ni mitungi maalumu na pia kuweza kuisafirisha kwa kutumia magari maalumu kwa ufanisi mkubwa. "

Gesi asilia iliyoshindiliwa ni mchanganyiko wa aina ya gesi za 'hydrocarbon' ambazo kiasi kikubwa katika mchanganyiko huo ni gesi nyepesi iiitwayo 'methane.'



Mhadhiri wa Chuo cha Usafirishaji (NIT) na Mtaalamu wa injini za gesi, Michael Kyando, akionyesha mpangilio wa mitungi ya gesi na namna inavyofanyakazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**SWALI:** Tuambie sifa za CNG kwenye matumizi ya magari.

**JIBU:** Ni nishati bora kwa injini za magari, huzifanya kuwa na ufanisi mkubwa na matumizi kidogo ya nishati. Aidha, huzalisha kiasi kidogo cha hewa ukaa (kaboni) zinazochafua mazingira. Pia kwenye injini haibakizi mabaki ya kaboni. Sifa nyingine ni kuongeza ufanisi wa nguvu wakati inapunguza kasi ya ulaji wa nishati.

**SWALI:** Tanzania ilianza lini kutumia gesi kwenye magari ?

**JIBU:** Kituo cha kwanza cha majaribio ya matumizi ya gesi kwenye magari kilijengwa mwaka 2009, eneo la Ubungo Maziwa nyuma ya mitambo ya kuzalisha umeme ya SONGAS na ndicho huweka gesi iliyoshindiliwa kwenye magari.

Aidha, pia ni kwa ajili ya kupata gesi iliyoshindiliwa na kuisafirisha kwa njia ya magari maalumu kwenda viwandani na katika taasisi ambazo hazipo kwenye mtandao wa gesi inayosafirishwa kwa mabomba.

Kituo hiki ni kikuu (mother station), kina mitambo ya kuchukua gesi asilia na kukandamiza kupata CNG na kinaendeshwa kwa ubia kati ya TPDC na kampuni binafsi PanAfrican Energy Tanzania (PAET).

Kwa sasa serikali -TPDC ina mpango wa kuongeza vituo vingi zaidi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja wengi. Aidha, ina mpango wa kushirikisha kampuni binafsi zikiwamo zenye vituo vya mafuta, ili kufunga pampu za kujaza gesi kwenye magari katika vituo vyao.

**SWALI:** Ni magari mangapi nchini yanayotumia CNG?

**JIBU:** Ni takribani magari 700 hadi sasa yamewekewa mfumo wa kutumia gesi asilia badala ya petroli au dizeli.

**SWALI:** Gari linalotumia CNG linapojazwa gasi linaweza kutembea umbali gani?

**JIBU:** Inategemea ukubwa wa injini ya gari hilo, kama ilivyo katika mafuta, magari yanatofautiana katika ulaji wa mafuta kutegemeana na ukubwa wa injini. Kwa mfano, kama gari linaweza kutumia lita moja ya petroli kutembea kilometa 10, vivyo hivyo litatumia kilo moja ya gesi kutembea kilometa 15.

Hivyo umbali ambao gari litatembea kwa kutumia kilo moja ya gesi ni zaidi ya mara moja na nusu ya ule ambao gari hilo lingetembea kwa kutumia petrol, hivyo kuna tija zaidi.

Baada ya kujaza gesi kwenye gari lililofungiwa mtungi wa kilo 15 kwa mfano, linaweza kutembea kati ya kilometa 220 hadi 280 kutegemeana na ukubwa wa injini na hali ya barabara.

**SWALI:** Ni faida zipi kimazingira zinazotokana na matumizi ya CNG kwenye magari?

**JIBU:** Mafuta ya petroli na diseli ni vyanzo vikuu vya uchafuzi wa mazingira ambavyo havijapata suluhisho la kudumu. Uchafuzi hutokana na oksaidi za kaboni, nitrojeni na chembe chembe ndogo sana zenye mchanganyiko wa kemikali hasa kwenye injini za dizeli.

Mifumo ya magari yanayotumia CNG, uzalishaji wa hewa ukaa hupunguzwa kwa asilimia 20 wakati utoaji wa chembe chembe (PM10) zinazochafua hewa haupo kabisa hivyo ni salama zaidi kwa mazingira.

**SWALI:** Kwa wastani gharama ya CNG ikoje ikilinganishwa na petroli?

**JIBU:** Nishati ya CNG huuzwa katika vituo maalumu vya kushindilia na kujazia gesi kwenye magari au CNG refueling stations na hupimwa kwa kilo. Mwaka 2020 kilo ya CNG iligharimu Shilingi 1,550 na inalingana au ni takribani lita 1.5 ya petroli. Kwa kifupi, matumizi ya CNG hutoa unafuu kwa anayetumia na yana faida kubwa kiuchumi kwa taifa.

Ujazaji wa gesi kwenye mtungi kati ya kituo kimoja cha kujazia gesi na kingine unaweza kuwa tofauti?

**SWALI:** Je, gari linaweza kutembea umbali tofauti tofauti kati ya ujazo mmoja na mwingine ilhali ukubwa wa mtungi wa gesi kwenye gari ni uleule?

Nini husababisha mabadiliko katika umbali ambao gari linaweza kutembea kabla gesi haijaisha kwenye mtungi tangu mtungi huo ulipojazwa gesi?

Kwa nini wakati mwingine umbali unaweza kupungua na wakati mwingine ukaongezeka kabla gesi kuisha kwenye mtungi ilhali ukubwa wa mtungi haujabadilika na gari ni lile lile?

**JIBU:** CNG siyo kimiminika kama petroli au dizeli, hivyo kiwango cha ujazo wa nishati hiyo katika mtungi hakitegemei tu ukubwa wa mtungi, lakini kiwango cha mgandamizo na jotoridi (temperature) ambalo linaweza kufikiwa wakati wa ujazaji wa gesi hiyo kwenye mtungi. Hivyo, kiwango kinachojazwa kwenye mtungi kinaweza kutofautiana kila wakati kutegemea na hali ya mgandamizo pamoja na jotoridi linaloweza kufikiwa wakati wa kuujazaji wa gesi hiyo kwenye mtungi wa gari.

Pia kiwango cha gesi inayoweza kuingia au kujazwa kwenye mtungi hutegemea sifa za gesi ambazo ni kubadilika kama vile uzito au mchanganyiko wake.

Sifa zinazoweza kuathiri kiwango cha gesi ambacho kinaweza kujazwa kwenye mtungi, mfano ikiwa nzito hupelekea ujazo mwingi zaidi wa gesi ndani ya mtungi.

Pia, utofauti katika umbali wa kutembea wa gari la CNG hutegemea namna ya uendeshaji wa gari, jinsi dereva anavyoendesha gari, hali ya barabara, pia kiasi cha gesi iliyojazwa mtungini.

Vilevile, ubora wa kufanya kazi wa injini pamoja na hali ya hewa ya wakati huo (mkandamizo wa hali ya hewa na unyevunyevu kwenye hewa), nao huchangia namna ya injini inavyofanya kazi.

**SWALI:** Gesi hujazwa kwenye gari kwa namna gani?

**JIBU:** Ujazaji hutumia bomba maalumu liitwalo nozzle kutoka kwenye pampu ya kujaza gesi (dispenser) inayounganishwa moja kwa moja kwenye 'valve' ya gari ya kujazia gesi ambayo mara nyingi hukaa juu ya injini ya gari hilo au karibu na eneo la kujazia petroli.

**SWALI:** Huchukua muda gani hadi kujaza mtungi?

**JIBU:** Huchukua kati ya dakika tatu na nne kujaza gesi kwenye gari la kawaida.

***ITAENDELEA***



## RC Mtaka, Mzee Malecela wateta

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amefanya mazungumzo ya masuala mbalimbali na Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, ikiwamo mikakati yake ya kuinua kiwango cha elimu mkoani humo.

Mtaka alimtembelea kiongozi huo nyumbani hivi karibuni jijini hapa na kumweleza vipaumbele vyake kwa Mkoa wa Dodoma.

Mkuu huyo alimwambia Malecela kuwa kipaumbele chake cha kwanza ni elimu na kazi iliyo mbele yake ni kunyanyua kiwango cha elimu na ufaulu katika Mkoa huo.

"Katika kuleta mabadiliko hayo ya elimu nimedhamiria kushirikiana na viongozi wazawa wa Mkoa wa Dodoma, wadau wote wenye jukumu la kusimamia elimu kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi ngazi za msingi hali kadhalika sekta binafsi," alisema.

Pia alitaja kipaumbele kingine ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuzifanya wilaya za pembezoni kuwa kanda maalum za kilimo na kukifanya cha mkoa huo kuwa cha kibiashara.

"Ni nafasi yangu pia kutilia mkazo kwenye zao la zabibu kama alama ya Mkoa wa Dodoma, alizeti na mazao mengine, matumaini yangu ni kuona kilimo kinasaidia kukuza uchumi wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma na kuwa mfano kwa wengine," alisema.

Mtaka alimweleza Malecela kuwa hali hiyo itasaidia kukidhi mahitaji makubwa ya mafuta ya chakula ambayo Tanzania imekuwa ikitumia fedha nyingi kuagiza mafuta nje ya nchi.

"Ni fursa kubwa ya kiuchumi kwa Mkoa wa Dodoma ambao mazao yanayotumika kuzalisha mafuta kama alizeti, karanga na ufuta yanastawi vizuri katika Mkoa wa Dodoma, lazima tutumie nafasi hii kuelekeza nguvu zetu katika kustawisha mazao haya kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo," alisema.

Kuhusu uboreshaji mazingira katika Mkoa wa Dodoma, Mtaka alisema ataendesha kampeni ya mkoa ya upandaji na ustawishaji miti kwa kuwashirikisha wadau wa ngazi mbalimbali kuanzia mkoa, wilaya, tarafa, kata, vijiji, vitongoji na ngazi za kaya.

"Mzee Malecela naamini utaendelea kunishauri vizuri kwa hili hasa ukizingatia wewe ni mwenyeji wa hapa na unajua hali ya hewa ya mkoa wa Dodoma, nipo tayari kupokea ushauri wako wakati wote ili kufanikisha kupanda miti mingi ili kuendana na azma ya serikali katika kuifanya Dodoma kuwa ya kijani," alisisitiza.

Kwa upande wake, Malecela alishukuru kwa mazungumzo hayo na kubainisha kuwa Dodoma ina fursa kubwa ya kilimo cha mazao yanayokamuliwa mafuta ya chakula .

Alizitaja Wilaya za Kongwa na Mpwapwa kama maeneo yenye hali ya hewa nzuri kwa uzalishaji wa karanga tangu miaka ya zamani na kwamba maeneo ya Wilaya zingine yanafaa kwa kilimo cha alizeti na zabibu.

# Askofu ataka tahadhari ya corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Covenant Faith Church Jerusalem Tanzania (CFCJ ), Damas Thadey, amewataka Watanzania kutopuuza maelekezo na miongozo inayotolewa na wataalamu wa afya juu ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Askofu Thadey aliyasema hayo katika ibada iliyofanyika Makao Makuu ya Kanisa hilo jijini hapa.

Alisema ni vyema Watanzania wakachukua tahadhari badala ya kusubiri kuona nchi ikiwa kwenye hali mbaya.

"Ugonjwa huu unaendelea kusambaa nchini, tuchukue tahadhari badala ya kusubiri tuone nchi inafikia hatua mbaya ya kuokota maiti mitaani," alisema.

Aliongeza: "Kwa mujibu wa serikali, kuwa wagonjwa wa corona wamefikia 408, huku wagonjwa 284 wakipumulia kwa msaada wa mashine, hivyo ninawaomba Watanzania wenzangu kujihadhari na hali hii."

Alisisitiza kuwa pamoja na kufuata maelekezo ya wataalamu, pia wasiache kumwomba Mungu ili kuwaepusha na ugonjwa huo.

"Tuongeze juhudi kwenye maombi ya kufunga na kuomba kwenye nyumba za ibada ili ugonjwa huu uondoke," alisema.

Aliwaasa viongozi wa madhehebu ya dini kuendelea kutoa elimu kwa waumini wao, jinsi ya kuepukana na ugonjwa huo kuanzia ngazi ya familia hadi kwenye mikusanyiko.

Alisema viongozi wa dini wana msaada mkubwa wa kuisaidia serikali kwa kupitia mahubiri yao ambayo yatasaidia kutoa elimu zaidi ya ugonjwa huo.

Awali, kiongozi huyo aliwahimiza waumini wake kuendelea kuiombea nchi ikiwamo na viongozi wake ili kulitumikia taifa kwa uaminifu na kuletea wananchi maendeleo.



Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camilius Wambura, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma jana, kuhusu taarifa za matukio ya ukatili na mauaji ya watoto na wanawake yanayoendelea kutokea maeneo mbalimbali nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijiji 305 vyapata mawasiliano ya simu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), umekamilisha miradi ya mawasiliano ya simu kwa kata 84 zenye vijiji 305 ndani ya siku 200 za Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Wizara hiyo wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 uliofanywa na Waziri Dk. Faustine Ndugulile.

Mashiba alisema miradi hiyo imenufaisha wakazi zaidi ya 700,000.

Aidha, alisema mfuko huo umekamilisha mradi wa kuboresha usikivu wa redio katika eneo la mradi wa kimkakati wa bwawa pamoja na maeneo ya Kisaki kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Zanzibar.

"Pia ndani ya siku hizo mfuko umefanikiwa kuanzisha kituo cha mawasiliano ya dharura yanayohitaji uratibu wa pamoja kama kutoa taarifa za matukio ya moto, mafuriko na magonjwa ya mlipuko kama vile COVID-19," alisema.

Hata hivyo, alisema hivi karibuni mfuko umetangaza zabuni mbili za miradi ya kufikisha mawasiliano katika maeneo ya mipakani na kanda maalum awamu ya sita.

Alifafanua zabuni ya kwanza ina kata 190 zenye vijiji 380 na imetengewa Sh. bilioni 26.83 huku zabuni ya pili ni mradi unaolenga kufikisha mawasiliano katika Ofisi za Halmashauri na kanda maalum ambapo imetengewa ruzuku ya Sh. bilioni 10.88 na utatekelezwa kata 34 zenye vijiji 45.

Alisema mradi wa kufikisha huduma ya mawasiliano mipakani unalenga kuhakikisha kuwa maeneo yote ya mipakani yanapata mawasiliano ya uhakika ili kulinda na kuimarisha usalama wa nchi.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mpango huo, Dk. Ndugulile alisema mpango umejikita kwenye nyaraka mbalimbali za kisera, malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa pamoja na Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2021-2025.



# Waomba uboreshaji ulipaji kodi za biashara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA jijini Mbeya, wameomba serikali kuendelea kuboresha mazingira ya ulipaji kodi ikiwa ni pamoja na usahihi wa ukadiriaji wa kodi hizo ili wafanye kazi zao kwa uhuru na kujiongezea kipato.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao wa masoko ya SIDO na Mwanjelwa walisema kwa sasa hali ya biashara imeanza kuimarika tofauti na ilivyokuwa awali ambapo ubabe ulikuwa unatumika kwenye ukusanyaji wa kodi hali iliyokuwa inawalazimu baadhi kufunga biashara zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Atupele Mwinuka, alisema tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alipotoa maelekezo wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), akitaka kuboresha mazingira kwa wawekezaji na wafanyabiashara hali imeanza kuwa nzuri.

Alisema tangu maelekezo hayo yalipotolewa, maofisa wa TRA wamebadilika na hakuna unyanyasaji tena kwa wafanyabiashara na hata lugha inayotumika ni rafiki kwao na inahamasisha kulipa kodi.

"Tulikuwa tukiwaona maofisa wa TRA tunafunga biashara na kukimbia, na ilikuwa inasababisha ukwepaji mkubwa wa kodi, walikuwa wakifika Mwanjelwa wenzetu wanatuambia kwamba wameshafika hivyo mjiandae, lakini sasa hivi hata wakikukuta hakuna shida, kilichobakia sasa hivi ni ukadiriaji wa kodi ndio unatakiwa kuboreshwa," alisema Mwinuka.

Naye Sajo Mwambipile, alisema kuna utitiri wa kodi ambao pia wanaiomba serikali izipunguze na kuongeza walipa kodi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wanajiita ni machinga, lakini uhalisia ni wafanyabiashara wanaostahili kulipa kodi kama walivyo wengine.

"Serikali ingefanya mpango wa kuhakiki upya biashara ili walipakodi tuwe wengi na viwango vipunguzwe, sasa hivi kuna watu wanajificha kwenye mwamvuli wa machinga, lakini biashara ziko vizuri kwa sasa hatukutani tena na vitisho vya maofisa wa TRA," alisema Mwambipile.

Hata hivyo, alisema biashara nyingi zimeyumba kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na kwamba ni vizuri serikali ikaangalia namna ya kuwapa nafuu zaidi wafanyabiashara kwenye ulipaji wa kodi.

# Mwalimu asimamishwa kazi tuhuma za kumtusi Rais

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

NAIBU Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amemsimamisha kazi mwalimu wa Shule ya Sekondari Momba, Shera Mwangoka, kwa tuhuma za kumtukana Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan.

Silinde alidai kuwa aliamua kujiridhisha kwa kuwahoji baadhi ya wananchi na walimu ambao walithibitisha kwamba imekuwa desturi kwa mwalimu huyo kutoa matusi mara kwa mara.

Alisema siku kadhaa zilizopita Mwangoka akiwa sokoni baada ya kuona Rais Samia kutangaza nyongeza ya mishahara na kupandisha madaraja kwa watumishi wa umma, alisema Rais alifanya hivyo kama hongo ili aungwe mkono na kudai ni mpumbavu kwa sababu ni mwanamke hawezi kumkubali.

"Nilipata taarifa mwalimu huyo kumtukana Rais nilianza kumuita mtu mmoja mmoja ili kujiridhisha kabla ya kuchukua hatua, wote walikiri na kudai kukerwa na tabia ya mwalimu huyo, serikali ya awamu ya sita hatuko tayari kufanya kazi na watu ambao hawako tayari kuheshimu mamlaka kwa hiyo kuanzia sasa nimemuagiza Ofisa Elimu wa hapa Momba, mwalimu huyo asimamishwe kazi kuanzia leo," alisema Silinde.

Alifafanua kuwa baada ya kusimamishwa kazi, hatua nyingine za kinidhamu zitafuatwa ikiwamo jambo lake kupelekwa kwenye Tume ya Utumishi wa Walimu na tume hiyo alisema anaisimamia yeye mwenyewe na hatua zitachukuliwa haraka.

Alisema mwalimu huyo ana mambo mengi ikawamo ulevi wa kupindukia, kutumikisha wanafunzi kubeba kokoto na anafanya hivyo ili akaziuze, kuwapa ujauzito wanafunzi na kudai anakabiliwa na tuhuma nyingi.

Aliwaambia wananchi kwamba serikali inawajali na kuwathamini walimu, lakini hawatakuwa tayari kufanya kazi na wenye utoro na utovu wa nidhamu hatua zilizochukuliwa kwa Mwangoka ziwe fundisho kwa wengine.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, alisema walipata ushahidi wa video ikionyesha mwalimu huyo akimtukana Rais.

Alisema walibaini suala hilo wakati wakifanya ziara ya kukagua shughuli mbalimbali za maendeleo katika Wilaya ya Momba ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, shule na miundombinu ya barabara.

Alisema katika ziara waliyoifanya wilayani Momba, walibaini asilimia 80 ya wananchi ambao walieleza vikwazo na kero zinazowakabili zilikuwa na ukweli na kuwaahidi kuzishughulikia.

"Haiwezekani mtu mmoja au kikundi cha watu kinamdhalilisha Rais Samia, wakati ndiyo anatunza na kuhudumia familia yako, natuma salama kwa watumishi wote wa umma ambao hawana nidhamu wanavunja miiko na maadili ya kazi zao mbadilike, kuweni makini vinginevyo tutaendelea kuielekeza serikali kuwachukulia hatua za kisheria," alisema Shaka.

"Kuna mwalimu alimtukana Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu kamwongezea mshahara, nilichukia sana nilitamani nimpige makofu nilichukia sana kwa sababu anamdhalilisha rais wetu kipenzi ambaye ametujali walimu kwa kuboresha mazingira yetu ya kazi," alisema Shaka.

Wananchi wa Wilaya ya Momba walisema kuwa baadhi ya walimu wameshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo badala yake huishia kunywa pombe kwenye vilabu na kuwadhihaki wananchi wa eneo hilo kwamba ni wapumbavu hawana akili.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, akivishwa mgolole na Mzee Michael Chalamila, aliyewasili katika shina namba moja Mkunywa, Kata ya Madibila, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya. **PICHA: CCM**

# Washauriwa kutumia mapato kujiunga CHF

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Sophia Kumbuli, amewashauri wananchi, kutumia sehemu ya mapato yatokanayo na shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kilimo na uchimbaji wa madini, kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF), kwa ajili ya matibabu wakati wanapougua.

Kumbuli alitoa ushauri huo juzi wakati akisikiliza kero za wananchi katika Kata ya Mbugani, wilayani humo na kwamba gharama ya kujiunga na mfuko huo ni Sh. 30,000 kwa kila kaya.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo huwa wanapata fedha nyingi hasa katika kipindi hiki cha mavuno na ni muhimu wakajiunga na mfuko huo ili uwasaidie kwenye matibabu wakati wanapokuwa hawana fedha.

Alisema kwa sasa lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wote wakiwamo wa sekta isiyo rasmi wanajiunga na bima ya afya ili kufikia lengo la afya bora kwa wote na kwamba ni muhimu wananchi hao wakachangamkia fursa hiyo.

"Mfuko huu unakusaidia wewe na familia yako kutibiwa katika hospitali yoyote ya umma isipokuwa hospitali ya rufani, sasa naamini mnapata fedha nyingi sana kwenye shughuli zenu, unashindwa nini kutenga Sh. 30,000 kwa mwaka mzima kwa ajili ya kulinda afya ya familia yako?" Alihoji Kumbuli.

Alisema afya ndiyo msingi wa uzalishaji bora wa mali kwa kuwa yeyote mwenye uwezo wa kuzalisha ama mtegemezi wake akiugua ni lazima shughuli za uzalishaji zitasimama ili kuhangaikia afya ya mgonjwa husika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, mpaka kufikia mwezi Desemba 2020 ni asilimia 2.2 pekee ya wananchi wote wa mkoa walijiunga na mfuko huo.

Dk. Manyatta alisema mfuko huo ulianza rasmi kutekelezwa katika mkoa huo Aprili 2019 na idadi kamili ya kaya zilizokuwa zimejiunga ni 8,949 zenye wanachama 37,528.

Alisema Halmashauri ya Busokelo ndiyo iliyokuwa inaongoza kwa kusajili watu wengi zaidi kwa kufikia asilimia 3.93, ikifuatiwa na Halmashauri ya Rungwe ambayo ilikuwa imesajili asilimia 3.15 huku Halmashauri ya Chunya ikishika nafasi ya tatu kwa kusajili asilimia 3.1.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilishika nafasi ya nne kwa kuandikisha asilimia 2.51, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambayo iliandikisha asilimia 1.76, Halmashauri ya Mbarali asilimia 1.62 na ya mwisho ilikuwa Halmashauri ya Kyela iliyokuwa imeandikisha asilimia 0.62.

Alisema uhamasishaji na uandikishaji wa wanachama wapya unaendelea katika halmashauri zote za mkoa huo na vifaa kwa ajili ya kazi hiyo vipo vya kutosha.

Kutokana na takwimu za Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuhusu idadi ya kaya zilizojiunga na CHF iliyoboreshwa, zinahitajika juhudi kubwa za kuhamasisha ili wananchi wengi zaidi wajiunge na kufikia lengo la serikali.



# ZAECA yatekeleza agizo la Rais uchunguzi wizi Shirika la Umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, (ZAECA), imeanza kufanyia kazi agizo la Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alilotoa kuhusu kufanya uchunguzi wa rushwa kwa watendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), wanaotuhumiwa kuchukua fedha za wananchi bila kuwapatia huduma ya kuwaunganishia umeme.

Ofisa Ufuatilia ZAECA, Ahmed Khamis Makame, alisema jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Rushwa barani Afrika.

Alisema ziara ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi katika mikoa mitatu ya Unguja, amepokea malalamiko mbalimbali ya wananchi kuhusu watendaji wa ZECO kupokea fedha kuunganishiwa umeme ikiwamo nguzo, lakini hawajapatiwa huduma hiyo.

"Ni kweli Rais ametoa agizo na kututaka kufuatilia kwa karibu sana tuhuma za watendaji wa ZECO na kazi hiyo tumeanza kuifanya," alisema.

Aidha, alisema jumla ya Sh. 411,348,724.3 zimeokolewa na kurudishwa serikalini baada ya tuhuma za ubadhirifu wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya serikali.

Alisema tangu Julai mwaka 2020 hadi Julai 2021, jumla ya malalamiko 532 yamepokelewa ikiwamo tuhuma 280 za rushwa na uhujumu wa uchumi, wakati majadala 29 yakiwa yamefungwa na kesi nne zimetolewa uamuzi.

Akizungumzia hali ya rushwa kwa upande wa Zanzibar, alisema ipo zaidi katika maeneo ya utowaji wa huduma za kijamii na vyombo vya sheria.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na mamlaka ya rushwa na uhujumu wa uchumi ni utoaji wa elimu kuhusu mapambano ya rushwa pamoja na kujenga uwezo zaidi kwa watendaji wa taasisi hiyo kwa sababu masuala ya rushwa yapo kiufundi zaidi.

"Tunaendelea na kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utoaji wa taarifa za rushwa kwa jamii pamoja na kujenga uwezo kwa watendaji wetu kuhusu njia ya kukabiliana na rushwa katika sekta mbalimbali," alisema.

Umoja wa Afrika mwaka 2018 ulitangaza kuwapo kwa maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Rushwa kutokana na athari zake ambazo hudhoofisha katika maeneo ya uwekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kiuchumi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard, wakati wa hafla ya kukabidhi mabati 255, mbao 220 na misumari kilo 100 vikiwa na thamani ya Sh. milioni 13 kwa ajili ya kuezeka Kituo cha Afya cha Jang'ombe kilichoko Wilaya ya Mjini Magharibi Mkoa wa Magharibi. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# SMZ yathamini viongozi wa dini kudumisha amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SEREKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema inathamini mchango unaotolewa na viongozi wa dini hali inayodumisha amani na utulivu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo kwenye mkutano uliojadili nafasi ya viongozi wa dini katika kudumisha amani na utulivu uliofanyika jijini Zanzibar.

Hemed alisema mchango wa viongozi hao kwa taifa umesaidia kustawisha maendeleo na kuchochea ustawi wa maisha ya wananchi.

Alisema uwapo wa amani na utulivu unaochangiwa na viongozi wa dini umesaidia kuwavutia wawekezaji tofauti jambo linalosababisha kupatikana kwa nafasi nyingi za ajira kwa jamii.

Alisema amani na utulivu inapaswa kulindwa na kila mtu na ikipotea serikali na taifa kwa ujumla itashindwa kupokea watalii na wawekezaji hatimaye kupunguza sehemu kubwa ya pato la taifa.

"Nawaomba viongozi wa dini na wananchi wote kwa ujumla tuendelee kudumisha amani na kila mmoja wetu aendelee kuwa mlinzi wa amani, utulivu na mshikamano wa nchi yetu," alisema Hemed. Kadhalika, alisema viongozi wa dini wamekuwa na moyo wa kijitolea katika kuhakikisha amani ya nchi inakuwapo muda wote kutokana na kazi nzuri waloifanya ya kuhakikisha inakuwapo kabla na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akizungumzia uwapo kwa maradhi mbalimbali, Makamu wa Pili wa Rais aliwapongeza viongozi hao kwa jitihada wanazozichukua katika kutoa elimu kwa waumini wanao waongoza kuchukua tahadhari dhidi ya Covid-19.

"Tumeshuhudia mchango mkubwa na mikutano mbalimbali mnayoifanya katika kupambana na maradhi ili kuhakikisha amani ya nchi hii haiteteriki," alisema.

Wakiwasilisha mada watendaji kutoka ofisi ya Mufti na Wizara ya Afya, walisema jamii inapaswa kufuata miongozo na maelekezo kutoka kwa viongozi ili kufahamu usahihi wa mambo kama ilivyoelezwa kupitia kitabu kitakatifu cha Qur-ani na mafundisho ya dini nyingine kupitia miongozo ya vitabu hivyo.

Akitoa salamu za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto Duniani, Naibu Mwakilishi wa UNICEF anayeshughulikia operesheni, Lawrence Ounndo, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Mufti kwa hatua wanazoendelea kuchukua katika kuwapatia watu taaluma kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo elimu ya kujikinga na kipindupindu, Covid-19 pamoja na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji.

Aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kutoa taaluma kwa jamii kutokana na uwezo wao wa kufikisha elimu kwa waumini wanaowaongoza.

Alisema UNICEF itaendelea kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na viongozi hao kwa kutoa msaada wao wowote ule unao hitajika kwa lengo la kufanikisha adhma ya kudumisha amani na utulivu pamoja na kupambana na magonjwa tofauti yanayoikumba jamii.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kabi, alisema taifa limejaaliwa rehema na baraka kutoka kwa Allah (S.W.) kwa kuwa na amani, jambo ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa waumini na wananchi kutekeleza ibada.

Aliwataka wananchi wa Zanzibar kusahau yaliyopita na kuepuka chokochoko zitakazo sababisha kusambaratisha kwa amani na utulivu miongoni mwa waumini wake.

# Wanaharakati waiomba ZEC usimamizi vyama vya siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAHARAKATI wa watetezi wa haki za wanawake, vijana na watoto wameitaka Tume ya Maadili ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ishirikishe wajumbe wengine kutoka sekta mbalimbali zikiwamo asasi za kiraia ili kuangalia, kujadili, kushauri na kupendekeza utendaji mzuri wa usimamizi wa mchakato mzima wa uchaguzi na mwenendo wa vyama vya siasa.

Uamuzi huo umekuja baada ya wanaharakati hao kufanya utafiti mdogo wa kupitia Sera ya Jinsia na Ujumuishi (Gender and Social Inclusion Policy) ya ZEC ya mwaka 2015 na kuona upungufu uliosababisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoshiriki ipasavyo katika mchakato wa chaguzi zilizopita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) kwa upande wa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, ametaka kuwapo na mwongozo maalum katika kila hatua ya uchaguzi kuanzia uandikishaji, utoaji wa elimu ya uraia, uteuzi wa wagombea, usimamizi wa uchaguzi, upigaji kura, utoaji wa matokeo na hali ya usalama, suala la usawa wa kijinsia na ujumuishi liongoze mchakato wote wa uchaguzi kabla, wakati na baada.

Alisema ili kuhakikisha usawa wa kijinsia na ujumuishi unafikiwa kwa kila ya hatua ya uchaguzi, ZEC inapaswa kukutana na wadau wa masuala ya jinsia, vijana na watu wenye ulemavu mara kwa mara ili kuona hali ikoje na kuweka mpango wa utekelezaji ili kusaidia katika ukusanyaji wa takwimu kama sera ilivyosema kuwa ZEC itakuwa na mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa takwimu (Systematically Data Collection).

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Salma Saadat, alisema pia katika utafiti wamebaini uwapo wa kamati ya maadili ya ZEC ni wa muda mfupi, huundwa wakati wa uchaguzi na uhai wake humalizika baada ya uchaguzi kwisha. Alisema pia kamati hiyo haijawekewa mwongozo wa kushughulikia malalamiko wala haina mwongozo wa kutatua vitendo vya udhalilishaji wanavyofanyiwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wakati wa uchaguzi.

"Kuna wanawake walifanyiwa vitendo vya udhalilishaji wakati wa uchaguzi, lakini hawajui waende wapi kupeleka kesi zao, kwa sababu kamati haina mwongozo wa kutatua kesi za mtu mmoja mmoja, kamati inapokea kesi za vyama vya siasa tu kwa mfano kesi ya ACT-Wazalendo kuhusu kiongozi wao kupinga kuwapo kwa kura za mapema ambapo alituhumiwa kuvuruga amani," alisema Salma.

Alipendekeza sera hiyo iweke mwongozo na mpango kazi ili ikidhi haja kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki ipasavyo katika mchakato mzima wa uchaguzi kama wapiga kura, wagombea, wafuatiliaji ilani na sera za vyama na hata kuhakikisha kuwa usalama wao unalindwa vyema.

Pia, alishauri Sera ya Jinsia na Ujumuishi ya ZEC ipitiwe tena pamoja na kuipangia mpango kazi ili iweze kutekelezeka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILIAN ONAEL KILEO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T 502 BCT** chasisi namba **ACA200013994**,engine namba **IA20196220**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/321818/2021**

116354502

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACQUELINE JOHN MPONELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0264/0041** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule yan secondary ya **BARBRO JOHANSSON** mwaka **2012**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa
**CONTROL NAMBA 9910820205254**

116354902

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEMA ROBERT MASSAWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0233/0039 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. MARYS MAZINDE JUU mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DAR/CHA/RB/343236/2021.**

116355002

## KUPOTEA KWA CHETI



**KAZIMIL JAMES** ANATANGAZA KUPOTEA KWA **CHETI CHAKE CHA KIDATO CHA NNE** CHENYE INDEX NAMBA **ME S 1750 -0045** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MTIHANI NECTA KUPITIA KASEME SEKONDARI MWAKA 2013.YEYOTE ATAKAE KIONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHA POLISI GEITA TAARIFA **RF/GE /TR /RB/3177/2021** AU APIGE SIMU NAMBA **0626 700029 /0693 789012 .**

116355102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TOWRISM DEV LTD** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 372 CQU** aina ya **SINORAY**. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,Taarifa ya jeshi la polisi, **KAH/RB/TR/360/2021.**

116355202

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABEID MBUYA MVUNGI ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 390 CRM AINA YA SUNLG RANGI NYEKUNDU. Kwa yeyote atakayeiona awasiliane na mhusika kwa namba 0717 989696 au aipeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu na yeye. Taarifa ya polisi: GEI/CHA/RB/346185/2021.**

116355302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCIS RAMADHANI SAMBUGUNI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU TIPPER** yenye namba za usajili **T388ARC** Lenye chases namba **FRR32D13003488** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/313967/2021**

116355902

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waziri awa mbogo kwa wawekezaji ranchi za taifa

**Na Mwandishi Wetu, MISENYI**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewaonya wawekezaji wanaohodhi vitalu vya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kinyume cha mikataba yao, kuachia mara moja ili kuwapisha watu wenye uwezo wa kuendesha shughuli ya ufugaji.

Waziri Ndaki, aliyasema hayo jana alipofanya ziara Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera kwa ajili ya kukagua Ranchi ya Mabale na kuzungumza na baadhi ya wawekezaji wenye mifugo waliopewa vitalu.

Aidha, Waziri Ndaki aliagiza kunyang'anywa kitalu kwa mwekezaji wa Kampuni ya Chobo Investment, baada ya kukaa muda mrefu bila kuendeleza.

Aliagiza eneo hilo kupewa wawekezaji wengine ambao wana mifugo waweze kulitumia, huku akimhakikishia mmiliki wa kampuni hiyo kupewa eneo kwenye ranchi nyingine ikiwa atafuata masharti ya mkataba.

Waziri Ndaki alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya wawekezaji kuchukua vitalu na kutovitumia kama ilivyoelekezwa kwenye mikataba na kusababisha maeneo kuwa mapori na kuvamiwa na watumiaji wengine wa ardhi.

Alisema, wizara yake kupitia NARCO imejipanga kuhakikisha wafugaji wanapata maeneo ya vitalu kwa ajili ya kufugia ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine.

"Wizara kwa sasa imejipanga kuhakikisha wawekezaji katika vitalu wanatumia maeneo hayo kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanalipa kodi kwa wakati," alisema Waziri Ndaki.

Alisema wizara kwa sasa inaiona NARCO kama ni sehemu ya kotokea kwani kupitia kampuni hiyo itaweza kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuongeza kipato kwa wafugaji.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia sekta ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema wizara imejipanga kuhakikisha uzalishaji wa mifugo na mazao yake unaongezeka na kuwasaidia wawekezaji wasikwamishwe katika kazi zao.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Misenyi, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Abdallah Mayomba, alisema uwepo wa ranchi katika wilaya hiyo imesaidia kupunguza migogoro ya ardhi.

Awali, baadhi ya wawekezaji walimweleza waziri huyo kuwa wanahitaji maeneo kwa ajili ya kufugia, na kuishukuru serikali kupitia NARCO kuwashushi gharama ya ukodishaji wa vitalu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Baobab ya Mapinga Bagamoyo wakifurahia na mwalimu wao wa taaluma, Edward Logiru, baada ya shule hiyo kufanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha sita yaliyotangazwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na wanafunzi wawili wa shule hiyo, Godwinner Joseph na Vailet Kahyoza kufanikiwa kuingia 10 bora kitaifa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Nyama ya Tanzania sasa kupata soko nje

**Na Joseph Mwendapole**

BIASHARA ya nyama kutoka Tanzania sasa itapata soko kubwa na la uhakika kwenye masoko ya nje baada ya Kampuni ya MICO International Halal Bureau of Certification (MIHB), kupata cheti cha kimataifa kitakachoiwezesha kutoa ithibati ya Halal.

Kampuni mbalimbali zilikuwa zikilazimika kupata ithibati ya Halal nje ya nchi kwa bidhaa zao, lakini kwa mara ya kwanza sasa Tanzania imepata kampuni iliyokidhi vigezo vya kimataifa vya ithibati ya Halal (MCO) ambaye ni wakala wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA).

Hafla ya kukabidhi cheti hicho ilifanyika mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Katibu wa Mufti ambaye alimwakilisha, Musa Bin Hemed na wawakilishi wa taasisi ya Uturuki iliyotoa cheti hicho ya Hafsa Halal Murat Bayka na Jalal Sahal.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Sheikh Mwenda Said, ambaye ni Mweka Hazina Mkuu wa BAKWATA, alisema cheti hicho kimetolewa baada ya baraza hilo kupitia mdau wake MICO International Halal Bureau Limited kuendesha mafunzo ya kuwaongezea wataalamu wao uwezo.

Alisema Hafsa Halal Certification and Food Import and Export Limited ya Uturuki kwa kushirikiana na MICO walianza kuwaongezea ujuzi watu hao kwa njia ya zoom kuanzia mwezi wa tatu mwaka huu na kuja kukamilisha mafunzo hayo ana kwa ana kuanzia Julai Mosi hadi sasa na wamefikia viwango vinavyotakiwa kimataifa.

Alisema wakufunzi hao wataendelea kutoa elimu ya Halal katika kila mkoa Tanzania Bara na ikilazimu pia wataenda Visiwani Zanzibar na kwamba MICO Halal imepata uwezo wa kutoa huduma za ithibati ya Halal kama nyama na bidhaa mbalimbali ndani ya nchi na kimataifa.

Akizungumzia umuhimu wa kuwa na cheti cha kimataifa cha Halal, Sheikh Mwenda alisema bidhaa za Tanzania zitakubalika katika soko la kimataifa hasa nyama na kuongeza pato la taifa litakalosaidia kukuza uchumi na kuongeza wigo wa ajira.

Alitaja faida nyingine kuwa ni bidhaa za Tanzania hususan nyama kukubalika kwenye soko la kimataifa kama uarabuni na barani Asia ambako huwa hawakubali bidhaa ambayo haina nembo ya Halal.

Alisema cheti hicho kitasaidia kuipatia nchi fedha za kigeni kwani kampuni za ndani zitakuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa mbalimbali ikiwamo nyama kwenye mataifa mbalimbali duniani.

"Nchi ilikuwa inapata hasara kwasababu makampuni ya ndani yalikuwa yanachukua ithibati ya Halal nje ya nchi kama Australia, Quatar na kwingineko, lakini sasa MICO Halal Tanzania itafanyakazi hiyo na hela zitabaki hapa nchini," alisema.

## Tigo yatoa mil. 220/- matibabu miguu pinde

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imetoa Sh. 220,000,000 kwa Hospitali ya CCBRT, kama sehemu ya kujitolea kwake kusaidia kituo cha afya katika kutokomeza tatizo la miguu pinde kwa Watanzania.

Mchango huu pia hutumika kama mpango wa uhamasishaji kwa umma juu ya umuhimu wa kufuata matibabu ili kuhakikisha wenye matatizo wanapona na kuzuia ulemavu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari, alisema: "Mchango wetu unathibitisha zaidi kujitolea kwetu kusaidia jamii zinazotuzunguka. Matibabu ya miguu pinde nchini ni mada ambayo inahitaji utangazaji na kama kampuni ya simu inayoheshimika, tuko hapa leo kubadili hadithi, tunahitaji ushiriki wa jamii na nguvu ya kuhakikisha kwamba kila mtoto aliye na miguu pinde Tanzania, anapata matibabu bora na kwa wakati kwa kutumia njia ya Ponseti, kama matibabu ya kiwango cha juu, hivyo kuwapa fursa sawa ya kuishi maisha yenye tija kama walivyo wengine."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi, aliishukuru Tigo kutokana na msaada huo endelevu ambao umekuwa ukisaidia kuokoa maisha ya watoto wengi Watanzania.

"Tigo Tanzania imeonyesha mfano kwa jukumu muhimu ambalo sekta binafsi imeamua kulichukua katika kuhakikisha inapunguza na kutatua shida za jamii.

"CCBRT, kwa miaka mingi imeweza kushughulikia moja ya mambo magumu zaidi ya matibabu ya miguu pinde, kuhakikisha matibabu yanakuwa endelevu na ufuatiliaji, kupitia uvumbuzi na msaada wa Tigo, kuna jukwaa la kukumbushana kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS), la CCBRT linaweza kutuma njia ya simu za mkononi kukuza ufuatiliaji ili wagonjwa watibiwe kikamilifu, bila athari yoyote.

Aliihimiza sekta binafsi kuendelea kuwapatia misaada ili kuhakikisha wanatokomeza tatizo hilo na kulimaliza kabisa.

Miaka mitatu iliyopita ya ushirikiano huu imeshuhudia karibu kesi 1,500 mpya za miguu pinde kwa watoto, wanaofaidika na matibabu ya miguu yanayobadilisha maisha kwa njia ya Ponset na mamia wamefanyiwa upasuaji CCBRT.

Alisema katika miaka ya hivi karibuni, kesi hizo zimezidi kupungua, na kwamba CCBRT inaendelea kufuatilia kwa ukaribu kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia malengo.

# RONALDO

## ATWAA KIATU CHA DHAHABU EURO 2020



**ROME, Italia**

CRISTIANO Ronaldo ameshinda tuzo ya kiatu cha dhahabu kwenye michuano ya Euro 2020 iliyomalizika juzi Jumapili.

Tuzo hiyo aliipata wakati Italia ilipoifunga England kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na kutwaa taji la Euro 2020 kwenye Uwanja wa Wembley.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, alimaliza michuano hiyo na Ureno akiwa amefunga mabao matano, sawa na straika wa Jamhuri ya Czech, Patrik Schick.

Lakini kwa sababu Ronaldo alikuwa na pasi moja ya mwisho kwenye mashindano hayo ikamwezesha kushinda kiatu hicho cha dhahabu kwa mujibu wa sheria za Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA).

Kwa mujibu wa sheria za UEFA kama wachezaji watakuwa na idadi sawa ya mabao, yule atakaye kuwa na 'asisti' nyingi ndiye anaibuka kinara.

Pia nyota huyo wa Juventus kwenye mashindano hayo aliweka rekodi mpya ya kuwa mfungaji mwenye mabao mengi zaidi katika michuano ya Ulaya akifikisha mabao 14 na kuipiku rekodi ya Michel Platini mwenye mabao 11.

## KANE: YEYOTE ANAWEZA KUKOSA PENALTI

**LONDON, England**

HARRY Kane amesema maumivu ya England kufungwa na Italia kwenye mikwaju ya penalti kwenye michuano ya Euro 2020 yatabakia kwake na wachezaji wenzake katika maisha yao yote ya uchezaji, lakini ameshauri wale wote waliokosa kama Bukayo Saka kunyanyua vichwa vyao juu.

Baada ya mchezo huo pale kwenye dimba la Wembley kumalizika kwa sare ya 1-1 katika muda wa kawaida na ule wa nyongeza, Kane alifunga penalti ya kwanza, lakini Marcus Rashford, Jadon Sancho na Saka walikosa.

Na hilo likawaacha England kushindwa kupata nafasi ya kubeba taji lao la kwanza kubwa kwa kipindi cha miaka 55, lakini Kane akasisitiza kikosi hicho cha kocha Gareth Southgate kipo katika njia sahihi kabisa.

Kane aliiambia BBC Sport: "Tusingeweza kujitoa zaidi, vijana hawakuwa tena na uwezo wa kujitoa zaidi.

"Penalti mara zote ni kitu kibaya unapokosa. Haikuwa bahati yetu.

"Yalikuwa mashindano ya kuvutia na najisikia fahari kwa hilo, hivyo wachezaji wote wanatakiwa kunyanyua vichwa juu kwa kile tulichokipata.

"Bila shaka najua kwamba itatuumiza kwa muda mrefu sana na itatuumiza kwa kipindi chote cha uchezaji. Nafikiri tutaweza kufanikiwa kwa mwaka unaofuata."



# RAJA CASABLANCA MABINGWA CAF



**CASABLANCA, Morocco**

KLABU ya Morocco, Raja Casablanca imefanikiwa kuchukua ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Js Kabylie FC ya Algeria.

Mabao mawili kutoka kwa Sofiane Rahimi na Ben Malango wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), yalitosha kabisa kuweka msumari wa moto kwa JS Kabylie.

JS Kabylie walifanikiwa kuingia katika fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2002, lakini bahati haikuwa kwao kutokana na ubora mkubwa ulioonyeshwa na Raja Casablanca.

Kutokana na ushindi huo, hivi sasa ni rasmi Raja ambao ni mabingwa wa kihistoria kutoka Morocco wamefanikiwa kuongeza idadi ya makombe ya Afrika mara sita.

Makombe mengine ni lile la Ligi ya Mabingwa Afrika ambalo wamechukua mara tatu na hili sasa wamechukua kwa mara tatu pia.

Itakumbukwa pia timu hii ilikuwa na wachezaji 10 uwanjani kutokana na mchezaji wao Victor Gomes kutolewa nje kwa kadi nyekundu, baada ya kumchezea vibaya mchezaji wa JS Kabylie.

HABARI MICHEZO

# Arsenal yasajili nyota wa Benfica

**LONDON, England**

BAADA ya kuwa na msimu mgumu wa 2020-21, Arsenal wanaonyesha ni jinsi gani msimu ujao hawataki utani na wanazidi kukiimarisha kikosi kwa kufanya usajili wa wachezaji mbalimbali wakati huu wa majira ya joto.

Washikabunduki hao wamekamilisha usajili wa beki wa kushoto, Nuno Taraves kutoka Benfica dili ambalo limetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 8.5.

Arsenal walitangaza tayari Nuno amesaini mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo.

Nyota huyo ataungana na timu ya Arsenal wiki hii baada ya kusafiri kutoka Ureno na kumaliza taratibu za kujitenga za kujinga na maambukizi ya virusi vya corona zilizowekwa na serikali ya Uingereza na atavaa jezi namba 20.

Akizungumzia usajili huo, Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta amesema wanamkaribisha Nuno katika klabu hiyo ili kuwa sehemu ya kusaka mafanikio.

"Tunamkaribisha Nuno katika klabu, ni mchezaji kijana ambaye amejizatiti na alipata maendeleo mazuri kule Benfica, pia alionyesha kiwango chake akiwa na timu ya taifa ya Ureno ya chini ya umri wa miaka 21.

"Ujio wa Nuno utaongeza nguvu katika kikosi chetu akiwa katika eneo la ulinzi hasa upande wa kushoto."






# BUKAYO, RASHFORD, SANCHO WABAGULIWA ENGLAND

**LONDON, England**

BUKAYO Saka, nyota wa Timu ya Taifa ya England baada ya kukosa penalti kwenye mchezo wa fainali dhidi ya Italia ya Euro 2020 amekuwa akiandamwa na mashabiki kwenye mitandao ya kijamii ambao wanaonyesha kila dalili za ubaguzi wa rangi.

Nyota huyo mwenye miaka 19 alitoka benchi na kupewa jukumu la kupiga penalti ya tano ambayo ilikuwa ni ya uamuzi pale kwenye Uwanja wa Wembley na alikosa na kuwapatia Italia ushindi wa 3-2.

Kipa wa Timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Donnarumma aliokoa juhudi za England ambao walikuwa wanahitaji taji hilo kwa kuwa imepita miaka 55 bila kutwaa taji na mwisho wa siku wakalikosa pia.

**Ripoti zimekuwa zikionyesha kuwa nyota huyo hana bahati kwenye mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na Instagram ambapo jumbe nyingi zinazoonyesha via shiria vya ubaguzi wa rang zimekuwa zikitumwa na kwenye akaunti yake pia amekuwa akikutana na meseji mbalimbali.**

Bahati mbaya pia wengine wamekuwa wakituma emoji kwenye mitandao ya kijamii katika posti ambazo aliziweka muda mfupi kabla ya fainali huku mmoja wa watumiaji alisema kuwa "Ondoka katika nchi yangu na mwingine aliandika kwamba, "Nenda Nigeria".

Mbali na Saka pia Marcus Rashford pamoja na Jadon Sancho ambao walikosa penalti nao wamekutana na jambo hilo.

Shirikisho la Soka la Uingereza (FA), limetoa taarifa kwamba itashughulikia suala hilo kwa kuwa sio la kimichezo.



# RONALDINHO AMTAJA NEYMAR MRITHI WAKE

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

NYOTA wa zamani wa Brazil, Ronaldinho Gaucho amemtaja mshambuliaji wa sasa wa timu hiyo, Neymar Jr kama mrithi wake kutokana na anavyojituma uwanjani.

Ronaldinho ambaye ni mshindi wa Ballon d'Or mwaka 2005 alikuwa nyota wa timu ya Brazil na akiisaidia kutwaa Kombe la Dunia mnamo 2002 na Copa America mnamo 1999.

Brazil ilitwaa Copa America ya 2019 wakati Neymar akiwa ameumia, na nyota huyo wa PSG alishindwa kuisaidia timu yake katika fainali Jumamosi wakati Argentina ilipoiadhibu Selecao hao bao 1-0 na kutwaa taji.

Ronaldinho anaamini kuwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amechukua nafasi yake kama shujaa wa Brazil, akiambia France Football: "Ndio, bila shaka, yeye ndiye mrithi wangu.

"Yeye ndiye mchezaji wetu mkuu, sanamu ya Wabrazil.

"Hajapoteza ujasiri wake, uchezaji wake, na daima ni raha kumwona uwanjani."

HABARI MICHEZO

## KWA UFUPI

**BENITEZ AMTAKA KOULIBALY**

KOCHA wa Everton, Rafa Benitez amewahimiza wakuu wa klabu kumsajili mlinzi wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly ambaye ni raia wa Senegal mwenye umri wa miaka 30. (***90min***)

**NAPOLI YAJIONGEZA**

KLABU ya Napoli inapanga kuwaachia Kalidou Koulibaly pamoja na kiungo wa Hispania, Fabian Ruiz, wakati wakijaribu kupunguza fedha zinazotumiwa kuwalipa mishahara wachezaji hao.***(Calciomercato)***

**MESSI KUBAKIA BARCA**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi yuko mbioni kusalia na Barcelona. Taarifa zinasema mchezaji huyo mwenye miaka 34 akitarajiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Katalunya. ***(AS)***

**JESUS ANUKIA JUVENTUS**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24 ni chaguo la kwanza kwa Juventus wakati wakitaka kuimarisha safu ya ushambuliaji msimu ujao. ***(Tuttosport)***

**ONANA AOTA MBAYA**

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili mlinda mlango wa Ajax, Andre Onana yamepata pigo baada ya mchezaji huyo kukubali masharti binafsi na Lyon. Klabu hizo mbili hazijafikia makubaliano. (***Fabrizio Romano - via Sun***)

**NEVES KUTUA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal wameanza mazungumzo na Wolves kwa ajili ya kumpata kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24. ***(Record)***

**CHIELLINI MAMBO SAFI**

MLINZI wa Italia mwenye umri wa miaka 36, Giorgio Chiellini atasaini nyongeza ya mkataba wa mwaka mmoja na Juventus wiki hii na kusalia na klabu hiyo ya Turin hadi Juni 2022. ***(Fabrizio Romano kwenye Twitter)***

**VIEIRA AINGIA SOKONI**

KOCHA wa Crystal Palace, Patrick Vieira anawania kumsajili, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 21 na mshambuliaji wa Denmark, Kasper Dolberg mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun)***

**DANJUMA HAUZWI**

KLABU ya Bournemouth imekataa dau la pauni milioni 13 kutoka Villarreal kwa ajili ya kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Arnaut Danjuma.***(Sky Sports)***

**BRENTFORD KUJIIMARISHA**

WAGENI wapya wa Ligi Kuu England, Brentford wanajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 10 ili kumnasa mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Wales, mwenye umri wa miaka 24, Harry Wilson. ***(Sun)***

**BELOTTI KUJIULIZA**

MSHAMBULIAJI wa Italia, Andrea Belotti mwenye umri wa miaka 27 ataamua ikiwa atasaini tena mkataba wake na Torino mara tu baada ya fainali ya Mashindano ya Euro 2020. ***(Sky Sport Italia)***



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MANCINI: NILITOA MACHOZI KWA SABABU YA WATALIANO

●●●Kocha huyo afunguka alikuwa na siku 50 ngumu za kupigania...

**LONDON, ENGLAND**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini amesema "nilikuwa na wakati wa furaha sana kwa hiki" baada ya kikosi chake kuifunga England kwa mikwaju ya penalti na kushinda Kombe la Euro 2020.

Mancini alishindwa kutwaa taji lolote kubwa akiwa mchezaji wa Italia, akimaliza nafasi ya tatu kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 1990 na nafasi ya pili kwenye michuano ya Ulaya chini ya umri wa miaka 21 mwaka 1986.

"Ilikuwa bahati kwangu kucheza katika kikosi bora mwaka 1990 na kile cha umri chini ya miaka 21," alisema.

"Licha ya ukweli kwamba tulikuwa timu bora, hatukufanikiwa kushinda na mara zote tulifungwa kwa mikwaju ya penalti."

Baada ya kushinda kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwaka 2018, Italia imefurahia wakati mzuri kwenye Euro 2020 chini ya Mancini, na hawajafungwa katika mechi 34.

Kocha huyo wa zamani wa Manchester City alisema machozi aliyoyatoa baada ya mchezo wa fainali hiyo yalikuwa ni kwa ajili ya Wataliano wote.

"Ulikuwa wakati wa aina yake kwangu kufanikiwa kupata kitu kikubwa. Ulikuwa ni wakati wa kuvutia kuona vijana wakishangilia na mashabiki jukwaani," alisema.

"Kuona kila kitu tulichokifanya kikifanikiwa, kazi yote ngumu tuliyofanya kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita imeleta hamasa kubwa.

"Na kwa hakika zilikuwa siku 50 za aina yake na ngumu sana kwa upande wetu, lakini tumeweza kupata kitu tulichokuwa tunakitafuta.

Italia wametwaa taji hilo la Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1968 na hiyo ni mara ya pili katika historia yao.

HABARI MICHEZO

# HATIMA YA METACHA YANGA KIZUNGUMKUTI

**Na Saada Akida**

HUKU zikiwa zimesalia mechi mbili kwa kila timu kumaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, uongozi wa Yanga umesema hatima ya golikipa wao, Metacha Mnata bado haijajulikana kwa sababu shauri lake liko mikononi mwa Kamati ya Nidhamu ya klabu hiyo, imefahamika.

Wakati Metacha bado jambo lake la utovu wa nidhamu likijadiliwa na kamati hiyo, tayari ya nahodha wa Yanga, Lamine Moro amerejea kikosini baada ya kukaa nje ya timu hiyo kwa muda mrefu kwa kilichoelezwa kosa la utovu wa nidhamu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema Lamine ameungana na wachezaji wenzake walioingia kambini juzi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Ihefu FC utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Bumbulia alisema baada ya viongozi, kocha wao, Nesreddine Nabi na nahodha huyo kukutana na kumaliza tofauti zao, sasa nyota huyo ameingia kambini ili kujiimarisha na kumalizia ngwe ya msimu huu iliyobakia baada ya kuukosa ubingwa watakwenda kukamilisha ratiba.

"Kesi ya Lamine imemalizika na suala la kucheza au kutocheza katika michezo iliyosalia ni jukumu la Nabi, kuhusu Mnata suala lake liko katika kamati husika na linaendelewa kujadiliwa, kwa sasa kipa huyo anatumikia adhabu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF)," alisema Bumbuli.

Metacha alifungiwa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, kwa kitendo cha kuashiria matusi katika mchezo wa ligi uliochezwa Juni 17, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa dhidi ya Ruvu Shooting ambapo timu yake iliibuka na ushindi wa mabao 3-2.

Baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Mnata aliwaonyesha mashabiki kidole cha kati ambacho ni ishara ya matusi na mbali na kufungiwa, kipa huyo ametakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000.

Yanga itashuka dimbani kuwakabili Ihefu ambao wako katika hatari ya kushuka daraja wakiwa na kumbukumbu nzuri ya kuwafunga watani zao Simba bao 1-0 katika mchezo wa kiporo uliochezwa Julai 3, mwaka huu wakati wageni hao kutoka Mbarali wao walitoka sare ya ugenini dhidi ya Kagera Sugar.

Kikosi hicho cha Nabi kitakamilisha pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwafuata wenyeji Dodoma Jiji FC, mchezo utakaochezwa Julai 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Tayari Simba yenye pointi 79 imeshatwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya nne mfululizo huku Mwadui FC ya mkoani Shinyanga nayo imeshashuka daraja.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake (Twiga Stars), wakiwa katika mazoezi kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mechi mbalimbali za kufuzu kushiriki mashindano ya Kombe la Afrika zitakazofanyika baadaye mwaka huu. **PICHA: TFF**

# KMC FC yawaita mezani Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC ya jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imetoa baraka kwa mchezaji yoyote wa timu hiyo anayetaka kujiunga na klabu nyingine kuondoka, lakini tu kwa kufuata taratibu za uhamisho zilizowekwa kisheria.

KMC imetoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa tetesi za beki wake wa kulia, Israel Mwenda anawindwa na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba huku Yanga ikiwa kwenye harakati za kunasa saini ya David Brayson anayecheza nafasi ya beki wa kushoto.

Meneja wa KMC FC, Walter Harrison alisema hayo jana jijini baada ya kuwapo kwa tetesi za klabu mbalimbali za hapa nchini zikiwamo, Simba na Yanga kudaiwa kuvutiwa na wachezaji wake.

"Milango iko wazi. Klabu yoyote ikimhitaji mchezaji yoyote waje katika mazungumzo, ingawa mpaka sasa hatujapata ofa yoyote rasmi kama kuna klabu inawahitaji wachezaji wetu," alisema meneja huyo na kuongeza.

"Hata klabu ikimtaka mtunza vifaa wetu au mimi mwenyewe hakuna shida, ili mradi taratibu zote zifuatwe. Kuhusu Mwenda huyu bado tuna mkataba naye, lakini hata hivyo bado haizuii kukaa pamoja na Simba kama wanamhitaji na Brayson huku mkataba wake unamalizika ligi ikiisha, naye tuko naye kwenye mazungumzo ya kumwongeza mkataba mpya, sasa kama kuna sehemu anataka kwenda, basi sisi hatuwezi kumzuia," Harrison alisema.

Kuhusu hatima ya timu hiyo, kiongozi huyo alisema baada ya ligi kumalizika watafanya usajili kwa ajili ya kupata wachezaji ambao wataifanya kuwa tishio na kuweza kushiriki michuano ya kimataifa kama ilivyowahi kufanya kwa mara ya kwanza walipopata nafasi hiyo.

"Tutahakikisha tunajiandaa kuwa na kikosi kizuri ambacho kitamaliza nafasi nzuri zaidi kuliko hiki cha msimu huu," aliongeza bosi huyo.

## Mtibwa yapania kubakia Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru amesema ana bahati na mechi za ugenini na moja ya mipango yake ni kuhakikisha anavuna pointi sita katika michezo miwili iliyosalia katika Ligi Kuu Tanzania Bara na kutimiza malengo ya kubakia kwenye ligi hiyo.

Badru aliliambia gazeti hili jana tangu alipotua katika kikosi cha Mtibwa Sugar amecheza mechi tatu ambapo ameshinda mbili na kutoka sare moja, huku kati ya hizo tatu amechukuwa pointi nne ugenini.

Kocha huyo alisema mbali na historia ya hizo mechi mbili, lakini amekuwa na rekodi ya kupata matokeo chanya kabla ya kujiunga na timu hiyo na anatarajia kuona nyota hiyo inaendelea katika michezo yake miwili iliyobakia ambapo ataanza kwa kuifuata Dodoma Jiji FC.

"Nina imani na mechi za ugenini huwa nafanya vizuri, kwa sasa nguvu na akili zetu tumezielekeza katika mechi hizo, tunajiandaa vizuri kupambana kutafuta pointi tatu dhidi ya Dodoma Jiji na kujiweka kwenye sehemu salama ya kutoshuka daraja," alisema Badru.

Alisema ana imani akipata pointi tatu katika mchezo huo wa keshokutwa kikosi chake kitaimarika na kujiweka nafasi salama ya kubakia kwenye ligi hiyo katika msimu ujao.

## Simba Queens kupewa kombe

**Na Saada Akida**

MABINGWA wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens wanatarajiwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Timu ya Taifa (Twiga Stars) itakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo aliliambia gazeti hili jana mechi hiyo imeandaliwa maalumu kwa ajili ya kuwakabidhi mabingwa hao kombe baada ya kufanikiwa kumaliza msimu wakiwa vinara.

Ndimbo alisema kuwa mbali na kuwakabidhi kombe la ubingwa, mechi hiyo itawasaidia Simba Queens kujiandaa na mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake ambazo zinatarajia kufanyika kuanzia Julai 17, mwaka huu.

"Kweli tumeandaa huo mchezo kwa maana mbili, kwanza kukabidhi kombe lakini kiufundi itawasaidia wawakilishi wetu ambao wanatarajia kuelekea Kenya katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo za Afrika kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati," alisema Ndimbo.

Simba Queens imepangwa Kundi A pamoja na Lady Dove ya Uganda na PVP FC kutoka Burundi wakati ndugu zao New Generation Queens ya Zanzibar wako Kundi B na Timu ya Benki ya Biashara ya Ethiopia na Yel Joint Stars ya Sudan Kusini.

# Michezo

Jumanne Julai 13, 2021

Nipashe




Mancini: Nilitoa machozi kwa sababu ya Wataliano HABARI UK. 22



Mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu (kushoto), akifunga bao huku beki wa Coastal Union, Paschal Kitenge akishindwa kuzuia hatari hiyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga: Tutapiga palepale

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba wakisherehekea kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya nne mfululizo, mabosi wa Yanga wanasisitiza wanajipanga kuhakikisha wanaibuka na ushindi mwingine dhidi ya watani zao katika mechi ya fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz aliliambia gazeti hili kwamba wao walimaliza msimu kwa kuwafunga katika mchezo uliofanyika Julai 3, mwaka huu lakini wamejiimarisha kuona wanaendeleza 'kilio' kwa watani zao watakapokutana kwenye fainali ya FA.

"Tunakwenda kuwapiga palepale kwenye mshono. Tulikutana nao Uwanja wa Mkapa bila wachezaji wenye majina na tukaamua mchezo kupitia Mauya (Zawadi), hamna namna sisi hatusemi sana ila tunatenda, tunajivunia mashabiki wetu ambao wapo pamoja nasi kila wakati," alisema Nugaz.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuendelea kushirikiana na wadhamini wao GSM ili kukamilisha jambo lao walililoiandaa kwa msimu huu.

"Tunasema tukutane Kigoma, huko ndio tutakamilisha jambo letu na msimu ujao kwenda katika mashindano ya kimataifa kwa tiketi yetu wenyewe," Nugaz aliongeza.

Yanga ilitangulia kutinga hatua ya fainali ya Kombe la FA kwa kuwafunga Biashara United kutoka Musoma wakati Simba ambao ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo waliilaza Azam FC.

# SIMBA YAWEKA REKODI MIAKA 42

## ●●●Huku Kocha Gomes akiwashukuru wachezaji, viongozi kwa kurahisisha kufikia malengo na...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetwaa ubingwa wa Tanzania Bara mara nne mfululizo ikiwa ni baada ya miaka 42 kupita, ukiwa ubingwa wa 22 tangu kuanza rasmi kwa mfumo wa Ligi Kuu ya Taifa ambayo ilianzishwa mwaka 1965.

Mara ya mwisho timu hiyo kufanya hivyo ilikuwa ni mwaka 1979, ilipotwaa ubingwa kwa mara tano mfululizo na haijawahi kufanya hivyo hadi juzi Jumapili usiku ilipoifunga Coastal Union mabao 2-0.

Simba imefikisha pointi 79 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ambayo imebakisha raundi mbili tu kukamilika.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Didier Gomes amesema Simba ilistahili kuwa mabingwa wa msimu huu na anampongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, ambaye ni Mwekezaji, Mohamed Dewji, Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez kwa kumpa nguvu ya kufanya kazi zake kwa utulivu hadi kufikia malengo hayo.

Gomes katika mafanikio hayo pia aliwasifu wachezaji wake kwa kutekeleza maelekezo yake kwa kiwango kikubwa kwenye mechi za mashindano yote waliyoshiriki msimu huu.

"Tulicheza vizuri na tulistahili kuwa mabingwa. Tumefurahi sana, ilikuwa ni kipaumbele changu cha kwanza, najivunia sana. Lakini huwezi kuwa kocha mzuri kama huna wachezaji wazuri pia, nawashukuru wachezaji wangu hawakuniangusha, ni kweli tumestahili kutwaa ubingwa huu," alisema Gomes.

Beki mkongwe kwenye timu hiyo, Erasto Nyoni alisema ubingwa huo walioupata ni furaha kwa Wanamsimbazi wote, huku akisema umoja wao ndiyo siri ya wao kutetea taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

"Kikubwa ni maandalizi, sisi tumekuwa na maandalizi mazuri, umoja na pia Mwenyezi Mungu anatubariki na tunaomba aendelee kutubariki," alisema Nyoni aliyejiunga na kikosi hicho msimu wa 2017/18 akitokea Azam FC.

Mpaka inatwaa ubingwa, Simba imecheza mechi 32, ikishinda michezo 25, ikitoka sare mechi nne na imepoteza mechi tatu.

Mabingwa hao wapya wamefunga mabao 73 na nyavu zao zimetikiswa mara 13, ikihitaji kufunga mabao matano ili kuweza kufikia rekodi ya msimu uliopita, ilipomaliza ligi ikiwa na magoli 78.

Ni msimu ambao Simba imekuwa bora zaidi kwenye kujilinda kuanzia kwa mabeki na makipa wao, kwani imeruhusu mabao 13 ikiwa imesalia mechi mbili, wakati msimu uliopita hadi ligi inaisha ilikuwa imesharuhusu magoli 21.

Baada ya kutwaa mara nne mfululizo mwaka 1979, Simba pia ilikuwa bingwa mwaka uliofuata wa 1980 na kulichukua kombe hilo mara tano mfululizo, kabla ya kulitema kwa watani zao Yanga mwaka uliofuata.

Simba pia iliwahi kutwaa ubingwa mara mbili mfululizo mwaka 1994 na 1995, pia mwaka 2003 na 2004, kabla ya msimu huu kuweka rekodi hiyo.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda alisema wachezaji wake wamefanya makosa ya kurudiarudia katika mechi mbalimbali walizocheza na hivyo juzi pia walistahili kuadhibiwa na Simba ambao walikuwa bora hasa katika kipindi cha kwanza.

"Soka ni mchezo wa wazi, wachezaji wangu wamecheza na timu kubwa ambayo ina wachezaji wenye uzoefu na uelewa mkubwa, tumeona jinsi ambavyo Simba walivyocheza katika mechi zao zote, nakiri kwamba walistahili kutwaa ubingwa msimu huu."

"Kipindi cha kwanza tuliruhusu mabao mawili baada ya hapo tulipokwenda mapumziko tukaelezana na hatimaye kipindi cha pili tulingia na mbinu nyingine na kuwazuia kutowapa nafasi ya kutufunga," alisema Mgunda.

Alisema mapungufu ya mechi dhidi ya Simba wanaenda kuyafanyia kazi na kuhakikisha wanapambana katika mechi mbili zilizosalia ili kuhakikisha wanapata pointi sita na timu yao kuendelea kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao.

Coastal Union iliyoko katika nafasi ya pili kutoka chini katika msimamo wa ligi, imebakiza mechi mbili za nyumbani ambapo keshokutwa itawakaribisha Mwadui FC na Jumapili itafunga pazia la msimu kwa kuwakabili Kagera Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >